Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

لا اله الا الله محمد رسول الله

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi watu! mcheni Mola wenu ambaye Amewaumbeni kutoka katika nafsi moja, na Ameumba kutoka katika nafsi ile nafsi yenzie, , na kutoka katika nafsi hizo mbili Akaeneza wanaume wengi na wanawake; na Mcheni Yeye bilkhususi kwa kuziheshimu fungamano za kidugu; hakika Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu yenu. (*4:2*).

JUZU 76 No. 189 | JAM2 /RAAJAB 1438 AH | MACHI 2017 | AMMAN 1396 HS | BEI TSH. 500/=

Khalifa Mtukufu awasihi Wanajumuiya

Zilindeni Ndoa sawa na Sunna za Mtume s.a.w.

Na Mwandishi Wetu, Dar es Salaam

Katika Hotuba ya sala ya Ijumaa ya tarehe 03/03/2017 Hadhrat Khalifatul V (Kiongozi wa waaminio duniani) aliwakumbusha wanajumuiya juu ya umuhimu wa kuzingatia miongozo ya Quran Tukufu na Sunna za Mtume s.a.w. katika maswala yahusuyo ndoa. Baada ya kusoma Tashahhud na Surat Fatihah, Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alisema:

Fungamano kati ya wavulana na wasichana na maswala ya familia yanayoibuka kati ya mume na mke yapo katika hali hii kwamba yanasababisha mazingira ya hofu na mashaka katika familia. Hii inaweza kuwa sababu sio tu ya matatizo ya wanandoa, bali pia inaweza kuwa chanzo cha hofu kwa pande zote mbili za wazazi.



Msikiti wa Baitul Futuh uliopo jijini London, ndio msikiti ambao kwa kawaida Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. hutoa hotuba zake za Ijumaa na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Huzur (atba) alisema kila siku ninapokea barua ambazo zimeandikwa kwamba wazazi fulani wameshindwa kumuozesha mtoto wao wa kike kwa kisingizio kwamba kwa sasa anasoma, ijapokuwa umri wake umepevuka. Kisha, anapoolewa wanashindwa kuwaelewesha kutokana na umri wao na mwisho wake ndoa inaishia kwenye talaka.

Jambo lingine wanalokutana nalo wasichana ni hili kwamba rafiki zao au baadhi ya wakati wazazi wao wanawahamasisha wasichana kwamba katika nchi hizi za Magharibi wanawake wana haki nyingi, hivyo wasichana hawa wawafanye waume zao wakubali matakwa yao. Huzur (atba) alisema kwa bahati

Endelea uk. 3

Jinsi Khalifa Mtukufu Anavyoguswa na Changamoto za Afrika

Na Jamil Mwanga, Dar es Salaam

Afrika ni miongoni mwa mabara yanayounda ulimwengu huu likiwa la pili kwa ukubwa wa maili za mraba zipatazo 11,700,000 sawa na asilimia 22 ya eneo lote la dunia. Historia inaonyesha kuwa bara hili limechangia kwa kiwango kikubwa maendeleo ya nchi za Ulaya, Marekani na nchi nyingine za dunia kupitia biashara ya watumwa ambapo nguvu kazi kubwa kutoka Afrika ilisafirishwa kwenda Ulaya na Marekani.

Ni ukweli usiopingika kuwa nchi nyingi za barani Afrika zinakabiliwa na changamoto nyingi za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Zimekuwepo jitihada kadhaa kuhakikisha kuwa bara hili linajikwamua katika hali hii ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika ambao moja ya majukumu yake ilikuwa ni kuhakikisha



Mhandisi Akram Ahmad Sahib, Naibu Amir Jamaat Uingereza na Mwenyekiti wa wa Taasisi ya Wahandisi na Wahandisi Majengo wa Kiahmadiyya, akiwaelezea wajumbe wa Majlis Amillah Taifa (hawapo pichani) kuhusu mafanikio ya miradi mbalimbali ya maji na umeme wa nguvu ya jua inayoendelea barani Afrika. Kushoto kwake ni Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry.

Bara la Afrika linaanza kupiga hatua kimaendeleo kwa kuhakikisha ustawi wa watu wake. Hata hivyo, imeelezwa kuwa Umoja huu umeshindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na kushindwa kupambana na nguvu za mabeberu kutoka nje.

Wapo wanaodai kuwa hali hii imesababishwa na sera za ndani za nchi nyingi za Afrika kujengwa kwa misingi ya kibepari badala ya usawa, upendo na mshikamano. Aidha, wapo waliokwenda mbali zaidi wakisema kuwa kitendo cha viongozi wa bara hili kulaghaiwa na kujiingiza kwenye mikataba ya kinyonyaji ni hali ya hatari na inayorudisha nyuma ustawi na maendeleo ya bara hili.

Ripoti ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2015 inafafanua kuwa uwepo wa umeme wa uhakika na wenye gharama nafuu

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KUMBE BADO

Ukiona bado una chembechembe za ushirikina (kumshirikisha Allah na kitu chochote). Kufikiri kwamba kuna mazingaombwe au nguvu za giza kuliko za Allah basi elewa kabisa ya kwamba hujajua bado kwamba Qur'an Tukufu iliteremshwa kwa mbora wa viumbe wote. Ukiona bado unaamini kuwa hoja na hekima havitoshi kumvuta binadamu kuingia katika Islam na unalazimika kutumia jambia, bunduki, n.k basi elewa fika una safari ndefu ya kuigusa Qur'an Tukufu. Ukiwa baado unavutiwa na utamu wa sauti tu bila kuzingatia ujumbe uliyomo katika maneno mateule ya Allah basi jua fika hujatafakari juu ya Qur'an Tukufu. Ukiwa na fikra potofu ya kufikiri Allah hasemi tena (Allah Apishe mbali) hivyo hazungumzi na waja wake, hatumi mitume wakati watu wake wamepotea, basi maizi kuwa umbali na Qur'n kama ilivyo mbali kutoka mbingu na ardhi. Na vilevile kama una uroho wa mali na pupa ya kukusanya fedha, dhahabu vinakushughulisha hadi unagaragara kwenye tope la riba – jambo ambalo ametangaza vita dhidi yake hapana shida hujawahi kufungua hata ukurasa mmoja wa Kitabu Kitakatifu. Kama hujawahi pia kujitupa kikweli kweli kwa Allah na ukaahidi kuwa mali yangu, uhai wangu na kufa kwangu vyote ni kwa ajili ya Allah basi ujue kuwa maskini hujui chochote kuhusu Qur'an Tukufu. Kama unahadaika na rangi yako ambayo hukufanyia jitihada yoyote kuipata, ukifikiri taifa lako, kabila lako, ukoo wako hivyo vyote ni bora kuliko wengine na katu hujatambua kuwa ubora wa mtu ni ukaribu alio nao na Allah na uwezo wa kujipaka rangi ya Taqwa basi wewe hujawahi hata siku moja kusoma hata aya moja wa kitabu hicho kitakatifu (Qur'an Tukufu).

Haya yote tuliyoyasema yanawezekana kabisa. Lakini tunachokulaumu nacho ni kwamba Mwalimu wa kufundisha Qur'an Tukufu tayari amekwishaletwa naye ni Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Tunachokuomba ufanye sasa ni wewe kuhudhuria katika darasa hilo. Kinachokukataza kuhudhuria darasa hilo ni nini? Wakati ziko dalili zote za kuonesha kwamba yapo mengine usiyoyajua kama tulivyofafanua hapo juu. Hujachelewa bado darasa hilo linapatikana katika vitabu takribani 80 vilivyoandikwa na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) ingawaje vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa vimeandikwa katika Kiurdu na Kiarabu na baadhi yake tayari vimekwishatafsiriwa katika lughaya Kiswahili.

Darasa hilo kwa sasa linaendeshwa na Makhalifa na Maulamaa wa Jamaat Ahmadiyya. La kufurahisha sana ni kwamba kila Ijumaa Khalifatul Masih V - Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) anatoa darasa ambalo tangu mwanzo hadi mwisho limejikita katika kufafanua Qur'an Tukufu. Tunatoa wito kwa ndugu wote watumie njia hizo tulizozitaja katika kuelewa na hatimaye kuigusa Qur'an Tukufu kwani ni Quran tukufu pekee inayoweza kutupa ufumbuzi wa matatizo yanayoukabili ulimwengu kwa hivi sasa.

Khalifa Mtukufu Anavyoguswa na Changamoto za Afrika

Kutoka uk. 1

kunachochea na kuharakisha kila nyanja ya maisha kijamii na kiuchumi. Hata hivyo, nchi zilizoko kusini mwa jangwa la Sahara zina tatizo la nishati linalohitaji kushughulikiwa haraka. Aidha, ripoti hiyo inasema kuwa waafrika wawili kati ya watatu, miongoni mwa takriban jumla ya waafrika milioni 621, hawana nishati ya umeme kabisa.

Kutokana na changamoto hizi zinazolikabili bara letu la Afrika, Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a kwa nyakati tofauti ameonyesha tena kwa vitendo namna ya kukabili changamoto hizi.

Akizungumza katika hafla ya Umoja wa Jumuiya ya Waafrika Waahmadiyya waishio nchini Uingereza katika kuadhimisha miaka 50 ya Uhuru wa baadhi ya nchi za Afrika, mwaka 2011 kiongozi huyo wa kiroho pamoja na mambo mengine alisema kuwa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya ilianzishwa mwaka 1889 na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian (a.s). Sisi Waahmadiyya tunamwamini yeye kuwa ni Masihi Aliyeahidiwa (a.s), Imamu wa zama na Mwonyaji.

Alisema kuwa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alitueleza shabaha kubwa za kutumwa kwake. Kwanza, kuanzisha na kuendeleza uhusiano kati ya mtu na Muumba wake lakini pili Mwanzilishi huyu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya alitumwa ili kumkumbusha mwanadamu kutambua wajibu alionao kwa wengine jambo ambalo kimsingi litapelekea kutambua thamani ya utu ambapo mwanadamu ataacha kuwa katili kwa mwenzie. Hivyo, mafundisho yake yakajenga msingi wa Amani ya kweli.

Tukiangalia hali ya kisiasa ilivyo duniani kwa sasa, tunaona kuwa kuna mifumo tofauti ya utawala ambapo kuna baadhi ya nchi udikteta ndio umeota mizizi. Katika nchi hizi raia hupewa haki finyu badala yake watawala ndio wanaokuwa na nguvu na kupata haki zote kwa maslahi yao. Matokeo yake ni watu wake kuishi katika hali ya mashaka, wasiwasi na kukata tamaa. Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ametufundisha na kutukumbusha mafundisho bora ya Islam ambayo yanasisitiza kujinyima kwa ajili ya kuwanufaisha wengine. Islam inafundisha ukarimu badala ya uchoyo. Islam inafundisha kwamba mtu mwema ni yule anayependa kuwatimizia wenzie haja zao zaidi kuliko za kwake. Pindi hali hiyo ya kujitolea inapokuwepo basi hapo hakuna ubishi wowote kuwa Amani ya kweli inapatikana. Wanajumuiya ya Waislam Waahmadiyya duniani kote mara kwa mara hujitolea michango ya fedha na misaada. Wanafanya hivyo sio kwa ajili ya kupata manufaa ya kidunia bali kwa lengo tu la kuwasaidia viumbe wa Mwenyezi Mungu.

Sambamba na hilo, Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) amesema kuwa miradi mingi mikubwa ya kibinadamu inatekelezwa barani Afrika. "Kwa msaada wa Allah, kwa miaka kadhaa sasa tumejitahidi sio tu kuwafanya Waafrika wawe karibu na Allah bali pia kutimiza wajibu wetu kwa watu hawa waishio kwenye bara hilo kubwa", alisema.

Ni katika muktadha huu, Jamaat imefungua shule nyingi barani Afrika. Ni katika hali hii hii wengi wa wahandisi wetu wa Kiahmadiyya ambao wamefundishwa na kukulia katika nchi za magharibi husafiri kwenda sehemu za vijijini barani Afrika kwa ajili ya kutoa huduma za maji kwa kuchimba visima na kuweka pampu kwa ajili ya wananchi masikini waishio katika maeneo ya vijijini.

Vivyo hivyo, Waahmadiyya wametoa huduma ya umeme kwa wananchi waishio maeneo ya vijijini barani Afrika kwa kuweka nishati ya umeme wa jua (solar panels).

Aidha, kwa sasa katika baadhi ya nchi kumeanzishwa mradi mpya wa kutengeneza vijiji vya mfano (model villages) ambapo hupatikana miundombinu kama maji ya bomba, umeme, taa za barabarani, huduma za mawasiliano ya jamii (community centres) na lami mitaani.

Vijana wetu wa Kiahmadiyya hufanya kazi hizi bila ya malipo. Kwa hakika hutumia

Endelea uk. 5



Nishati ya nguvu ya umeme wa jua zilizofungwa katika Kituo cha Jamaat Eneo la Kitonga, Dar es Salaam ambayo husaidia katika matumizi mbalimbali ikiwemo pampu za kusukuma maji katika visima vilivyochimbwa kwenye eneo hilo.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Zilindeni Ndoa sawa na Sunna za Mtume s.a.w.

Kutoka uk. 1

mbaya kwa kuona uhuru na starehe zilizopo katika nchi hizi, hadi wasichana kutoka Pakistan wameanza kudai mahitajio yasiyokuwa ya msingi.

Huzur (atba) alisema baadhi ya wavulana wenye urafiki na uhusiano na mtu mwingine na wanadhamira ya kuwaoa, lakini wanakuwa na hofu kuwaeleza wazazi wao juu ya hayo mwisho wanaishia kuwaoa binamu zao au kuoa katika familia za marafiki zao huko Pakistan. Baada ya muda wanaanza kuwanyanyasa wasichana wasio na hatia na wanawatendea kwa dhuluma. Huzur (atba) alisema katika kesi kama hizi, bila shaka ni watoto ndio ambao wanaathirika kiakili na kisaikolojia.

Huzur (atba) alisema ufunguo wa kusuluhisha matatizo yote haya yanayojitokeza unaweza kupatikana ikiwa kama mtu atageukia katika imani. Tuna bahati nzuri kuipokea imani na baraka zile za mafundisho yaliyoletwa na Masih Aliyeahidiwa (a.s). Moja ya mafundisho hayo ni kutanguliza dini (imani) zidi ya mambo yote ya kidunia. Inapokuja katika swala la ndoa hadi wale waliojitolea kwa ajili ya kuitumikia dini wanasahau kanuni hii muhimu, ambapo Mtukufu Mtume (s.a.w) alitoa muongozo maalumu kuwa ikiwa kama utahitaji kuingia katika maswala ya ndoa basi mtu utangulize imani dhidi ya mambo mengine ya kidunia.

Hazrat Khalifatul Masih I (r.a) alisema jambo la kwanza ambalo Islam imelisema kuhusiana na Nikah (ndoa ya kiislam) ni hili kuwa lengo la ndoa liwe kwa ajili ya kuimarisha imani ya mtu badala ya kutafuta uzuri, utajiri na hadhi. Vile vile kabla ya mtu kuingia katika ndoa ni lazima afanye Istikharah (hii ni sala kwa ajili ya kupata matokeo mazuri ya jambo lolote).

Aya zinazosomwa wakati wa sherehe ya ndoa zinaweka msisitizo juu ya maombi. Ingawa zaidi ya hivyo, katika kipindi cha kufunga ndoa Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa anafanya maombi kwa ajili ya kuwaombea baraka wale walioingia katika fungamano hilo la ndoa. Hivyo, ndoa inatakiwa ipate utulivu kwa kuombewa yale yalio bora kwa pande zote na kuomba baraka za Allah juu yake. Ijapokuwa wapo baadhi ya watu kutoka Pakistani na India ambao bado wanaendeleza tamaduni zao na wanatoa kipaumbele katika mambo ya makabila na familia wakati wa kuchagua mwenza kwa ajili ya ndoa, wakati Mwenyezi Mungu Mtukufu alisema mtu anatakiwa atangulize imani kwanza juu ya yote.

Kwa hakika, tunatakiwa kuzingatia ombi la posa hasa ndani ya familia husika ingawa sio lazima. Masih Aliyeahidiwa (a.s) aliwahi kuulizwa kuhusiana na mtu kukubali posa ya ndani ya familia na Masih Aliyeahidiwa (a.s) alisema ni bora zaidi kufanya ndoa ndani ya familia ikiwa mwenza mzuri anapatikana lakini sio lazima kufanya hivyo.

Baadhi ya wakati, wanawake wanalaumiwa na kudhihakiwa kwa kutotoa zawadi za kutosha. Watu hawa wanatakiwa waangalie mfano wenye baraka wa Mtume (s.a.w) kuhusiana na mambo haya na namna gani alivyowaoza mabinti zake kwa kufanya mambo kiurahisi wakati wa kutoa zawadi. Vile vile familia ya bibi harusi isijipe mzigo mzito wenyewe na watoe zawadi ambayo wanaweza kuimudu.

Kabla ya kufanya maombi ya Istikhara, wanaotaka kuoana ni lazima waonane. Mtukufu Mtume (s.a.w) alimuelekeza mmoja wa sahaba zake kwenda kumuona anayetaka kumuoa kabla ya kufunga ndoa. Hivyo, hakuna ubaya kwa mvulana pamoja na familia yake kwenda kwenye nyumba ya msichana na kuonana nae. Ijapokuwa, zipo baadhi ya familia za wavulana ambazo zinaonyesha hali ya majivuno wanapotembelea nyumba ya msichana na wanatoa maoni ya kuchukiza. Pia wanakawia kutoa majibu ya kukubali kwao na ikiwa katikati litatokea ombi lingine zuri zaidi basi wanalikubali hilo na kuachana na la kwanza.

Ikiwa kweli mtu aelewe lengo la ndoa basi wanawake hawawezi kuwa na hisia za uchungu na hakuna mvulana ambae angeonyesha hali ya majivuno. Masih Aliyeahidiwa (a.s) alisema lengo haswa la ndoa ni kumlinda mtu dhidi ya zinaa, kulinda utimamu wake wa kimwili na kupata kizazi chema.

Baadhi ya wakati, sababu ya kutoelewana ndani ya ndoa ni kwa sababu mume hana nyumba ya kuishi mwenyewe na hivyo anaishi pamoja na wazazi wake. Wakati mwingine hili linaweza kuwa ni kwa sababu mume ana shida ya kifedha au bado anasoma na hivyo sio rahisi kwake kuwa na nyumba yake binafsi. Katika hali kama hiyo mke anatakiwa kumsaidia na aishi na wakwe zake hadi mume apate uwezo wa kununua nyumba yake. Katika baadhi ya wakati, wanawake na waume zao wanavunja ndoa zao, hivyo jambo hilo sio sahihi kabisa. Ikiwa kama msichana hawezi kuishi na wakwe zake anatakiwa kuhairisha jambo hilo tangu mwanzo. Ijapokuwa wapo baadhi ya wanaume wanaoishi pamoja na wazazi wao kwa mambo wasiyo na wajibu nayo bali wanatafuta kisingizio cha kutaka kuwasaidia wazazi wao.

Hazrat Khalifatul Masih I (ra) alisema baadhi ya watu hususani wanaoishi katika nchi za India wanalalamika kuhusiana na migogoro kati ya mke na mama mkwe majumbani. Ijapokuwa, kama watu washikamane na mafundisho ya Quran, basi migogoro ya aina hiyo isingetokea kwa sababu Quran tukufu imeeleza kwa uwazi kwamba kila mmoja akae katika nyumba yake.

Huzur (atba) akaongezea kwamba kwa upande wa familia ya binti wapo wanaouliza kama kijana ana nyumba yake na ikiwa hana basi hawashughuliki na posa yake. Pia jambo hili sio sahihi kwa sababu mwisho wa siku kijana anapata uwezo wa kuwa na nyumba yake, lakini ndoa ni lazima ifungwe kwa kutanguliza Taqwa (Ucha Mungu) na sio viwango vya kidunia. Vile vile, baadhi ya familia hawawaozeshi watoto zao kwa Wabashiri kwa sababu wamejitolea maisha yao kwa ajili ya dini.

Kisha, Allah Mwenyezi Amewaamuru wanaume ndani ya Quran Tukufu kutofanya haraka kujibu kama wake zao wanasema kitu na wala wasiwatendee kinyume cha wema. Allah Mwenyezi Anasema:

"…. Na kaeni nao kwa wema, na kama mkiwachukia, basi huenda mchukie kitu mbacho Allah Ametia kheri nyingi ndani yake" (4:20).

Akielezea aya hii, Hazrat Khalifatul Masih I (ra) anasema kwamba kwa kutumia njia nyingi Mwenyezi Amewashauri wanaume kuwatendea wake zao kwa wema na wanaume ni lazima daima walikumbuke hili.

Jambo jingine ambalo ni chanzo cha kuleta mitafaruku ni pale wanaume wanapoamua kuoa mke wa pili. Lakini, ingawa Islam imeruhusu kuoa mke zaidi ya mmoja lakini kuna baadhi ya masharti na hali. Bila shaka sio kwa ajili ya kukidhi tamaa ya mtu.

Kuhusiana na hili Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba sheria ya Mungu Mwenyezi isitumike kinyume na shabaha yake, na wala isitumike kama kinga kwa ajili ya haja binafsi. Kufanya hivyo itakuwa ni dhambi kubwa. Mungu Mwenyezi Amerudia mara kwa mara kuasa dhidi ya kuendeshwa na tamaa za mwili. Ucha Mungu pekee ndio uwe mshawasha wako kwa kila kitu.

Ingawa Mungu Mwenyezi ameturuhusu mambo mengi ya kidunia, hilo halimaanishi kwamba tutumie maisha mazima kujikita katika hayo kwa wingi. Kwa mfano, tusitumie muda wetu wote, nguvu na nadhari kwa kukaa na wake zetu tu. Kwa hilo ndoa zetu zitakuwa na maana ya kushirikisha na Mungu kama sawa, kwa kuwa Quran inasema sifa ya mtumishi wa Allah ni kwamba "wanapitisha usiku mbele ya Bwana wao, wakiinama na kuinuka" Kwa kifupi tunahitaji kujiepusha na kuweka nguvu zetu zote katika kutimiza tu matamanio ya kidunia kwa kuacha kujenga mshikamano wa karibu zaidi na Allah. Ingawa Mtume Mtukufu (SAW) alikuwa na wake wengi lakini alikuwa akitumia usiku wake mzima katika ibada.

Masihi Aliyeahidiwa (as) kisha akasema:

"Kumbukeni vizuri kwamba Utashi hasa wa Mungu ni kwamba msizingirwe kabisa na tamaa na kwamba kuifanya taqwa yenu iwe kamili, kama haja ya kweli imetokea, oeni tena (msingi hasa wa kuoa mara ya pili ni taqwa). Hivyo kuoa tena imeruhusiwa. Hata hivyo wale wote wanaotaka kuoa kwa mara ya pili wanahitaji kujichunguza kwamba wanafanya hivyo kwa misingi ya Taqwa au kwa sababu ya haja zao zilizojaa tamaa?"

Kisha Masihi Aliyeahidiwa (as) akasema:

"Kumbukeni kwamba anayeoa mke zaidi ya mmoja kwa sababu tu ya tamaa za nafsi na za kimwili yuko mbali na kiini cha kweli cha Islam. Ni dalili ya kuangamia kwa mtu kama katika kila siku inayochomoza na kila usiku unaoanguka, yeye hakutani na matatizo na mateso na hayuko tayari kupata maumivu yoyote bali anataka maisha ya raha na "analia kidogo au halii kabisa na anacheka zaidi."

Masihi Aliyeahidiwa (as) amewashauri wanawake kwamba kama waume zao wanataka kuoa tena kwa sababu nzuri, wasipinge. Lakini wanawake wanaruhusiwa kuomba kwamba Allah Mwenyezi kwanza Asiwafanye wakutane na shida ya aina hiyo. Wanaume pia wameshauriwa kwamba wasioe tena kwa sababu tu ya haja za matamanio, bali msingi wake uwe taqwa pekee.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anaendelea kuelezea zaidi kwamba wanawake mara nyingi wanaliona swala la uke wenza katika Islam kwa mwanga hasi na hawana imani katika suala hili. Kwa mfano kama mke akipatwa na wendawazimu, au akipatwa na maradhi yanayomfanya asiweze kufanya kazi, na mume hawezi kubaki mvumilivu katika useja, itakuwa si haki kwa uwezo wa mwanamume kutomruhusu kuoa tena.

Wakati Mungu Ameacha wazi mlango Wake kwa wanaume kutegemeana na hali fulani, Mungu pia Ameacha wazi mlango kwa wanawake kwamba katika hali zisizoweza kuzuilika anaweza kuomba Khulla kwa kupitia mamlaka muwafaka kama kwa mfano mume amekuwa hawezi kufanya kazi.

Sheria ya Mungu ni kama duka la dawa ambalo linatoa matibabu kwa magonjwa yote. Kama sharia ya Mungu ingekuwa haina fursa hii ya ndoa ya pili kutatua hali za aina fulani, isingekuwa duka lenye ufanisi.

Injili inaruhusu talaka kwa uzinzi tu lakini inashindwa kutambua idadi isiyohesabika ya magomvi mengine yanayoweza kutokea kati ya mume na mke hivyo kuacha mahusiano yakipata pigo kali. Hata hivyo Masihi Aliyeahidiwa (as) amewahakikishia wanawake na kusema msikhofu kwa sababu Kitabu mnachokifuata hakitegemei kukisia, na kinatunza haki za wanawake kama kinavyofanya kwa wanaume.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anaeleza kwamba mke anaweza kupata Khulla kutokana na useja wa mume. Hata hivyo badala ya kulalamika kwa Mungu wakati mume wake anataka kuoa tena, ni lazima awe mcha Mungu na hivyo Mungu Atamfanya mume wake mcha Mungu. Sharia imeruhusu ndoa ya pili kwa mume kwa sababu fulani halisi, lakini kama mke hawezi kuvumilia kuifuata Amri hii ya sharia, asilalamike kwa Mungu, bali badala yake akate rufaa kwa Kudra ya Kimbingu kwa maombi kwani Kudra ya Kimbingu iko juu ya Sharia. Aombe kwamba Kudra ya Kimbingu igeuzie mbali na mawazo yote yale yaondolewe kutoka kwenye fikra za mumewe ya kuoa tena. Masihi

Endelea uk. 4

Zilindeni Ndoa sawa na Sunna za Mtume s.a.w.

Kutoka uk. 3

Aliyeahidiwa (as) anasema kama ataomba hili kwa dhati ya moyo basi pengine uwezekano wa mumewe kuoa tena kamwe hata hauwezi kuinuka.

Huzur (atba) alimalizia kwa dua ndefu ambayo muhtasari wake ni kwamba Wanajumuiya wote wanaume kwa wanawake watatue matatizo yao ya nyumbani kwa kutegemea Amri za Kimbingu. Zaidi ya hapo matatizo yote yawe yenye kuondolewa kutoka kwenye ndoa mpya kwani matatizo mengi yanazuka. Na kwamba wote waelewe madhumuni ya kweli ya ndoa sio kutimiza haja za kimwili, bali kutoa kipaumbele kwa imani na kukilinda kizazi kijacho.

Huzur aliongoza sala tano za jeneza, mbili mwili ukiwepo na mbili ghaib.

Sala ya jeneza ya kwanza ilikuwa ni ya Muhammad Nawaz Momin Sahib, Waqif-e-Zindagi (aliyejitolea waqfu maisha yake). Ni mjukuu wa sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Baba yake alijaza Baiat mwaka 1922 chini ya mkono wa Hazrat Musleh-e-Maud (ra). Mwanzoni watoto wa baba yake walikuwa wakifa wakati wakizaliwa na wasio Waahmadiyya walikuwa wakimcheka kwa hilo. Nawaz Mumin alipozaliwa baba yake alimuomba Mungu kama atapona atamtoa wakfu maisha yake kwa Islam. Matokeo yake akapona na maisha yake yote aliyatumia katika njia hiii. Alihitimu Jamia Ahmadiyya na alifanya kazi katika ofisi za Al-Fazal, Darul Qazaa na Wasiyyat. Mwaka 1969 alikwenda Ujerumani na alifanya kazi kule. Alikuwa ana jazba kubwa ya kuhubiri, alikuwa akisali daima katika wakati na alikuwa akifunga saumu, alikuwa mvumilivu sana na mwenye shukurani. Alikuwa na mapenzi yasiyo na mipaka kwa Quran Tukufu. Ameacha binti mmoja na mtoto mmoja wa kiume. Alikuwa ni Muusi.

Sala ya jeneza ya pili ilikuwa ya Syed Rafiq Safir Ahmad Sahib wa Uingereza ambaye alikuwa ni raisi wa Jamaat ya Surbiton. Baba yake alikuwa ni Dokta Safiruddin ambaye alikuwa ni Mkuu wa kwanza wa Shule ya Sekondari ya Ahmadiyya Kumasi, Ghana. Rafiq Safir Sahib aliitumikia Jamaat tokea utotoni na maisha yake alitumikia katia vyeo vya katibu wa Atfal, Qaid Khuddam na katika ngazi ya Makao makuu katika Ansarullah alikuwa Qaid Seht-o-Jasmani na Qaid Amoomi. Cheo chake cha mwisho alikuwa raisi wa Jamaat ya Surbiton. Alikuwa ni Muusi, alikuwa na uhusiano wa kina na Ukhalifa, alikuwa akisali sala za Tahajjud, alikuwa ni mcheshi na mchangamfu, na alikuwa na asili ya upole sana ucha Mungu na unyenyekevu. Mke wake anaandika kwamba kutokea siku wameoana mpaka amefariki alikuwa akijishughulisha kuitumikia Jamaat. Alikuwa akiwakumbusha watoto wake sala kwa upendo na ki wajibu. Alikuwa akitatua matatizo ya watu na kuwasadia kifedha. Kaimu raisi wa Jamaat moja anasema moja ya tabia zake nzuri ilikuwa ni baada ya sala ya Isha alikuwa akiwauliza watoto maswali kuhusu kila hotuba ya Ijumaa, na alikuwa akiwapa zawadi kwa majibu sahihi, hivyo kupenyeza hamu ya hotuba kwa watoto. Ameacha mabinti wawili na watoto wa kiume wawili.

Sala ya tatu ya jeneza (ambayo ilikuwa ya kwanza ya jeneza ghaib), ni ya Dokta Mirza Laiq Ahmad Sahib, mtoto wa kiume wa Sahibzada Hafeez Ahmad Sahib. Alikuwa ni mjukuu upande wa baba wa Hazrat Musleh-e-Maud (ra). Ninamuomba Allah Ampe nguvu mama yake ambaye bado yuko hai. Mbali na elimu zingine alipata MBBS yake kutoka katiko chuo cha tiba huko Multan. Alikuwa akifanya kazi Rabwah na alikuwa makini sana kwa watu masikini. Wale waliokuwa masikini wamesema wao wenyewe, kwamba aliwaonyesha huruma ya hali ya juu. Alitenga siku moja nzima katika wiki kutibia masikini bure kabisa. Ndoa yake ya kwanza ilikuwa na Syeda Faiza Sahiba aliyezaa nae watoto wawili wa kiume. Ndoa yake ya pili ilikuwa na Amatul Shakuur Sahiba, binti wa Hazrat Khalifatul Masih III (ra). Ninamuomba Allah Mwenyezi Amjaalie marehemu Baraka na Msamaha. Amin

Sala ya ya pili ya jeneza Ghaib ilikuwa ni ya Mheshimiwa Ameenullah Khan Sahib, mbashiri wa zamani huko Marekani. Marehemu aliwezeshwa kufanya kazi ya ubashiri huko Marekani, Liberia na Uingereza. Tokea utotoni wazazi wake walimtoa maisha yake waqfu kuitumikia Jamaat, kutokana na ombi la Khalifatul Masih III (ra). Mwaka 1949, baada ya kumaliza elimu yake ya kati alijiunga na Jamia Ahmadiyya. Mwaka 1955 alimaliza elimu yake ya Maulvi Faazal. Kutokea tarehe 29 Februari mwaka 1960 mpaka Aprili mwaka 1963 aliwezeshwa kufanya kazi kama mbashiri huko Marekani. Mara yake ya kwanza kutumwa Marekani ilikuwa ni mwaka 1960 alipokuwa na umri wa miaka 23. Alikuwa ni mbashiri mwenye shauku kubwa. Alipata fursa nyingi kuhubiri kupitia magazeti na redio. Wakati akifanya kazi huko Liberia alikuwa akialikwa kwenye mikutano ya kila mwezi na alikuwa akiambiwa aongoze maombi ya kimya. Wakati Khalifatul Masih III (ra) alipotembelea Liberia basi chakula cha usiku kiliandaliwa kwa heshima ya Huzur na mwenyeji alisema kumhusu Ameenullah Khan 'Ana nguvu sana', Huzur (ra) alijibu 'Ana nguvu bila kutumia nguvu yoyote' Ameenullah Khan Sahib alipelekwa pia Uingereza ambako alifanya kazi mpaka mwaka 1970. Kisha ilimbidi kustaafu kutokana na afya dhaifu. Alimuoa Bushra Sahiba, binti wa Iqbal Shah Sahib, na mjukuu wa Walayat Shah Sahib, sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa (AS).

Huzur (atba) aliomba kwamba Allah Mwenyezi Anyanyue vyeo vya marehemu wote. Amin.

Magomeni Mikumi Wafanya ziara ya Kimalezi

Na Ahmad A. Nasibu.

Ama kweli penye wengi hapaharibiki jambo! Moja kati ya faida nyingi zinawozekana kupatikana kutokana na kufanya vikao ni kuibuliwa yale tunayoghafilika nayo mara kwa mara. Wazo la kufanya matembezi ya malezi kwa wanajamaat wenzetu liliibuliwa mwisho wa kikao chetu cha tawi cha kuchagua ajenda na mjumbe wa Shura kwenye kipengele cha mengineyo. Sote kwa pamoja tulitikisa vichwa vyetu kuashiria kukubaliana na wazo hilo lililotolewa na mjumbe mwenzetu.

Jumamosi ya 11 Machi wajumbe wanne wa majlis ya tawi ambao ni rais wa tawi bw. Mwinyimvua M. Ussi, katibu wa tawi bw. Mohammed mwinyimvua, Katibu wa Tabligh wa tawi bw. Suleiman Mubarak na Katibu wa fedha wa tawi bw. Ahmad A. Nasibu tuliifanya ziara hiyo na kuzifikia kaya tano. Ziara hiyo ilianza tawini nyumbani kwa marehemu Abdulrahim Nasibu majira ya saa 3 ya asubuhi mara baada ya safu ya ziara kukamilika.

Ujumbe ulizuru maeneo ya Mwananyamala, Tandale, Magomeni Kimamba,



Kulia: Mohammed Mwinyimvua – Katibu wa tawi, Suleiman Mubarak – Katibu wa Tabligh, Mwinyimvua M. Ussi – Rais wa tawi, Mzee Ramadhan Shamte na Ahmad A. Nasibu – katibu wa fedha.

Magomeni Mikumi na Kinondoni Mkwajuni ambapo wanatawi husika wanaishi. Tulipata nafasi ya kuona uhalisia wa maeneo ya kuishi ya wanatawi wenzetu na changamoto zinaweza kupatikana katika malezi ya wanafamilia wao. Ukumbusho juu ya kushika maagizo ya Jamaat kwa nguvu zote haswa sala na yale yanayotolewa na Huzur a.t.b.a katika kila hotuba zake za Ijumaa, ulitolewa. Suala la kujitolea katika mali na wakati pia lilitiliwa mkazo wa namna yake kwa pamoja na ujumbe wote.

Sehemu ya mwisho ya ziara yetu ilikuwa ni nyumbani kwa Mzee Ramadhan Shamte pale Kinondoni Mkwajuni. Tulipasahau kidogo maana 'njia haina alama', lakini ile sifa ya mhubiri na mshairi huyu maarufu ajulikanaye na vijana kwa wazee kama "*Mke si Mali*" hadi mtaa wa tatu ilitusaidia kufika bila ya kupepesa tena macho. Nje ya nyumba yake pana bango kubwa lenye maandishi yasomekayo "Mke si Mali", kisha na ufafanuzi unafuatia juu ya maana ya mke, mahari, watoto, mali n.k. linalofanya utoe tabasamu kwa furaha. Tulipata kumjulia hali ya maendeleo ya afya yake ambayo bado haijatengemaa kwa muda mrefu sasa. Moja ya maneno ambayo nayakumbuka kama mfano wa shukrani yake juu ya hali aliyo nayo ambayo aliyasema baada ya kuuliziwa hali yake ni " roho haijambo, lakini mwili unakataa kukubaliana nayo". Maneno hayo yalikuwa kichwa cha habari cha mikasa yote aliyotusimulia.

Ama kwa hakika inatupasa kudumisha desturi hii aliyotufundisha yule Mtumishi wa Rahmani, mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. ya kutembeleana si tu katika ugonjwa na shida bali kwa kudumu kwa ajili ya udugu wetu. Kwa hakika ilikuwa ni ziara ambayo iliamsha ari za wanajamaat tuliopata kuwatembelea na kwetu tuliokuwa wajumbe wa ziara hiyo. Tunachukua fursa hii kuwahimiza na kuwatoa hofu wana-majlis wengine wa matawini juu ya kufanya matembezi ya kimalezi kwa wanatawi wao kadiri ya wasaa kwa faida ya Jamaat zao husika. Tutimize wajibu wa kukumbusha Wanajamaat wenzetu kwani kila mchungaji ataulizwa juu ya kile alichopewa kukichunga.

Kila sifa njema ni za Allah, Mola wa ulimwengu.

Chimbuko la Jina Tanganyika

Na Mahmood Hamsini Mubiru
Safarini Kigoma

Katika kitabu changu 'Nani aliyebuni Jina Tanzania' nilikiri kutofahamu ni kwa jinsi gani jina Tanganyika lilivyopatikana. Hata mwalimu Julius Jambarage Nyerere aliwahi kukiri pia ya kwamba ingawaje yeye alikuwa anapenda sana mambo ya utafiti lakini hakubahatika kufahamu lilipochimbuka jina "Tanganyika". Kukiri kwamba unajua kwamba hujui ni ule utamadauni tuliofundishwa na Allah ya kwamba '*Kwa kila Anayejua yupo anayejua zaidi*'.

Safari yangu ya utafiti ya Historia ya Ahmadiyya mkoani Kigoma imenisaidia sana na kunifungua macho kwani nilibahatika kukutana na Mwanajumuiyya Bw. Juma Iddi Abedi ambaye elimu yake juu ya historia ya Kigoma sio tu kwamba ni pana bali ni ya kujivunia. Bwana Juma Iddi Abedi ni mwanahistoria katika maana halisi ya neno hilo. Na wale wote wanaohitaji kuifahamu historia ya Kigoma na makabila yaliyomo katika mkoa huo wanashauriwa kukutana na Bw. Juma Iddi Abedi.

Ni masikitiko makubwa katika jamii yetu kitu wanachohusudu sana ni makaratasi na vyeti kuliko kile mtu anachokijua kichwani. Ni lazima ikumbukwe kwamba katu hatudharau vyeti kwani navyo vina nafasi yake, tunachokisema ni kwamba si busara hata kidogo kumaizi ya kwamba kuna njia moja tu ya kupata elimu. 'Wahyi', Uzee, Simulizi za wazee zote hizi ni njia ya kupata elimu. Na hatuna haki hata kidogo ya kudharau njia hizo. Ukimsikiliza kwa makini Juma Iddi Abedi akichambua makabila ya Mkoa wa Kigoma utaikumbuka ile methali ya Kiswahili isemayo; "Avumaye baharini ni Papa, lakini wengine wapo". Hapana shaka kwamba Bw. Juma Iddi Abedi ni mweledi wa historia ya Kigoma na utakapomsikia akiwachambua na kuwatoa makosa baadhi ya watafiti na waandishi wa vitabu walioandika juu ya Kigoma ndipo utaheshimu umahiri wake juu ya historia ya mkoa huo. Masikitiko yetu makubwa hata hivyo ni kwa kiasi gani wajuzi wa namna hii wametambuliwa na kupewa ukumbi ili kuonesha vipaji vyao?

Bw. Juma Iddi Abedi mara baada ya sala ya Ijumaa nilimuuliza juu ya kuwepo kwa duka la vitabu hapo Kigoma, kwani mimi nilikuwa nimezunguuka dari madari (sehemu zote) sikufanikiwa kuliona duka la vitabu isipokuwa vitabu vya mashuleni tu. Kabla hajanijibu nilimuonesha kitabu nilichonunua TMP Bookshop Tabora kiitwacho "*Waha – Historia na Maendeleo*" kilichoandikwa na P. Chubwa. Bw. Juma Iddi Abedi alisema ya kwamba alikuwa amekisoma kitabu hicho na kwamba kilikuwa na upungufu mkubwa mno kwani kilikuwa kimejaa upotoshaji na kutobanga historia nzima ya wenyeji wa Kigoma. Sawa na Juma Iddi Abedi Waha sio watu wa kwanza kufika Kigoma. Wao ni wageni na walipokelewa kwa huruma na mapenzi na wenyeji. Upotoshaji wa mambo ni kwingi katika kitabu hicho alisema Bw. Juma Iddi Abedi. Na alisema ni kosa kufikiri ya kwamba aliyetoa jina la Tanganyika ni Gavana wa Kikoloni wa kwanza H. Byatt. Bw. Juma Iddi Abedi anajenga hoja na kusema ya kwamba jina Tanganyika limekuwepo kabla ya ujaji wa wavamizi na wote wanaoishi kando kando ya ziwa hilo ambalo ni lenye kina kirefu kuliko maziwa yote duniani walilifahamu kuwa ni ziwa Tanganyika.

Kuhusiana na chimbuko la jina Tanganyika; Bw. Juma Iddi Abedi anaainisha nadharia tatu:-

NADHARIA YA KWANZA – LUGHA.
Waarabu walipofika Ujiji waliwakuta Waha na kuwauliza wenyeji wako wapi? Wale Waha waliyoulizwa waliwambia kwa lugha yao; "Mukitanga Mumnyika" maana yake wako kwenye bonde lenye maji. Ni dhahiri ya kwamba ipo desturi jina kubadilika sawa na wakati na matamshi na hususan wageni wanashindwa kutamka vizuri. Kwa mathalani Tabora ni "Ntobora" ikiwa na maana ya viazi. Dodoma ni Idodomya maana yake ni kudidimia. Unguja "Ungo wajaa" kuna kipindi mavuno yalikuwa mazuri huko Zanzibar na hivyo likapatikana jina Unguja. Huko Unguja pia kuna sehemu inaitwa "Kizimkazi" na linatokana na Bwana mmoja aitwaye Kizi ambaye alikuwa akienda na kurudi Mzizima ambayo ni Dar Es salaam ya sasa. Hatimaye kutokana na kuwa na mazoea hayo wakawa wakimuita jina la Kizi mkazi. Na eneo hilo mpaka leo linaitwa kwa jina hilo hilo la 'Kizimkazi' kufuatilia mtiririko wa mawazo hayo ni dhahiri Waarabu waliposikia "Mukitanga Mumnyika" wakashindwa kutamka maneno yote hayo na kurahisisha wakachukua maneno ya mwisho ya kila neno na likazaliwa Tanganyika.

NADHARIA YA PILI – SAMAKI WAWILI 'TANGA' & 'NYIKA'.

Ziwa Tanganyika lina maajabu makubwa. Ni ziwa lenye kina kirefu kuliko maziwa yote Duniani. Ni ziwa pia lenye samaki aliye na umeme. Maajabu hayo yaliwasisimimua wengi na wakataka wayaeleze kwa wengine. Na ndipo linapatikana jina Tanganyika. Ni ziwa lenye samaki anayeingia kwa hiyari kwenye mtumbwi wakati samaki wengine wanakimbia. Samaki huyo anaitwa Tanga. Tanga ana desturi ya ajabu yeye huruka kwenye mtumbwi. Hiyari si utumwa. Na kaburure si ugonjwa (Ugonjwa wa kujitakia). Sidhani kwamba kuna sehemu yoyote ile duniani alipo samaki wa aina hii. Lakini anayeelewa kwamba yupo atusaidie. Samaki mwingine ana umeme yeye haitaji msaada wa Tanesco. Akishikwa akawekwa na samaki wengine wanakufa. Anao umeme. Maajabu haya yote yanapatikana katika ziwa lenye samaki wawili wa ajabu, Tanga na Nyika na hapo ndipo inakuwa rahisi kusema tunakwenda wapi? Tunakwenda kwenye ziwa lenye samaki wawili, Tanga na Nyika.

NADHARIA YA TATU – MZIMU
Makabila ya Kongo ambayo hivi leo ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo yanaamini kuwa katika maji hayo kuna mzimu ambao hufurahi na kukasirika. Unapofurahi mzimu huo hurusha samaki ufukweni na watu wanajiokotea. Mzimu huo unaitwa Tanganyika. Ni vizuri tukalitazama suala la mizimu katika Afrika kwa uangalifu mkubwa. Tujihadhari kuwa na pupa. Tunaanza na hoja ya kwanza kwamba Allah ametuma mitume kwa watu wote. Inawezekana kabisa dawa hizi za kienyeji zilifahamishwa kwa Nabii. Alipofariki wakaleta biashara na udanganyifu katika dawa hizo.

Inawezekana kwamba jambo lenyewe lilianza kwa haki na kweli lakini taratibu ukaingia mkono wa binadamu ambao siku zote huharibu na kuchafua. Isiwe haya matambiko na uchafuzi ni mafundisho yaliyokuwa sahihi na miaka ilivyokwenda ikaingia dosari na upotoshaji. Dini hivi leo zimeingiza upotoshaji tena upotoshaji wa kusikitisha mno. Binadamu kumfanya Mungu na mwingine mama wa Mungu (Mwenyezi Mungu Apishe mbali). Miujiza ya Abdulqadir Jilani inatisha na kumvika kilemba kisicho chake. Hoja yetu ni kwamba, si ajabu mizimu hiyo tunayoisikia yalikuwa mafundisho ya Nabii na kwa sasa yamekwishachafuliwa. Kuna haja kubwa ya kufanya uchunguzi sahihi katika mila hizo na desturi za Waafrika. Nakumbuka wasomi kutoka Afrika ya Magharibi walimtembelea Khalifatul Masihi wa IV - Hadhrat Mirza Tahir Ahmad (rh) naye akawaomba wafanye utafiti katika mila na desturi za Kiafrika asaa wakapata mambo mengi ambayo yanahusiana na Unabii katika Afrika. Maagizo hayo ya Khalifa wa Allah ni muhimu kwani elimu ni bahari kuu katu hufiki pwani.

Maelezo hayo yote kwa ujumla yanatusaidia kwa njia moja au nyingine kufahamu ni kwa jinsi gani nchi yetu Tanganyika ilivyopata jina lake.

Khalifa Mtukufu Anavyoguswa na Changamoto za Afrika

Kutoka uk. 2

fedha zao wenyewe kushiriki katika miradi hii kwa sababu wanapenda kutimiza amri ya Allah ambayo ni kuwahudumia binadamu na kutimiza haki kwa viumbe.

Khalifa Mtukufu (a.t.b.a), Hadhrat Mirza Masroor Ahmad ambaye amewahi kuishi Ghana kwa zaidi ya miaka minane, anayafahamu fika mazingira na tabia za Waafrika. Anasema kuwa kwa jumla, Waafrika wanapenda kujitolea ili kuwasaidia marafiki na ndugu zao.

Mwenyekiti wa Wahandisi Majengo atembelea Tanzania

Katika kile kinachoonekana kuwa ni juhudi ya Khalifa Mtukufu V a.t.b.a, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad kuwasaidia wananchi wa bara la Afrika kukabiliana na changamoto za huduma za kijamii na kiuchumi hususan maji na umeme, hivi karibuni alimtuma hapa nchini Mhandisi Akram Ahmad Sahib kwa ajili ya usimamizi na utekelezaji wa miradi hii ya kibinadamu.

Mhandisi Akram sahib ambaye ni miongoni mwa Manaib Amir wa Jamaat ya Uingereza ndiye Mwenyekiti wa Taasisi ya Kimataifa ya Wahandisi na Wasanifu Majengo wa Kiahmadiyya. (*International Association of Ahmadi Architects and Engineers* - **IAAAE**)

Mhandisi Akram sahib anabainisha kuwa alianza kutumikia taasisi hii tangu Huzur (a.t.b.a) alipochaguliwa kuwa Khalifa mwaka 2003. Alisema kuwa awali Huzur (a.t.b.a) alisimulia uzoefu wake alipokuwa akiishi barani Afrika katika nchi ya Ghana kuna kipindi yeye na familia yake walikuwa wanatumia maji kutoka mtoni na hivyo kupata magonjwa yanayotokana na maji kwa muda mrefu. Hata mwandishi wa makala haya aliwahi kushuhudia Huzur (a.t.b.a) akisimulia kupitia televisheni ya MTA-Afrika akisema kuwa wakati akiwa Ghana kama Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Ahmadiyya aliishi katika maeneo ya vijijini ambako sio tu usafiri ulikuwa wa tabu bali kulikuwa hakuna umeme, maji wala gesi achilia mbali maji ya mtoni ambayo upatikanaji wake nao ulikuwa ni wa shida. Mhandisi Akram sahib anasema aliagizwa na Huzur (a.t.b.a) kushughulikia changamoto hizi lakini kwa gharama nafuu.

Akielezea mafanikio yaliyopatikana kupitia miradi ya maji na umeme wa jua (solar power), Mhandisi Akram sahib alisema kuwa badala ya kutumia teknolojia ghali kutoka Marekani, wamefanikiwa kuweka umeme wa jua kwa kutumia teknolojia rahisi kutoka China katika vijiji vipatavyo 250 barani Afrika ambako sasa watu wanatazama televisheni ya MTA kwa kutumia umeme wa jua. Kama hiyo haitoshi, hadi sasa tayari visima 2000 vimeshachimbwa katika maeneo mbalimbali Afrika ambapo timu ya wataalam hujitolea muda na hata nauli kuja Afrika kwa ajili ya kusambaza huduma hizi muhimu na za msingi kwa binadamu. Takribani vijiji 15 vya mfano (model villages) vimeanzishwa Afrika ambapo wahandisi takribani 60 wanafanya kazi ikiwemo katika nchi za Afrika Magharibi za Ghana na Nigeria.

Kwa hapa Tanzania tayari huduma za visima vya maji zilizofungwa pampu zanazotumia umeme wa jua zinapatikana katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika eneo letu maarufu la kituo cha Jamaat lililoko Kitonga, Kata ya Msongola Wilaya ya Ilala nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam. Maeneo mengine ni pamoja na Chuo cha Jamia Ahmadiyya, Kihonda mkoani Morogoro na Msikiti wa Dodoma.

Bustani ya Washairi

KADI TAMATI AHADI,
KADI YAATI MAHADI (AS)

1. Najikinga kwa Rabani, Allah Aliye Azizi,
   Anilinde na Shetani, Apigwaye kama jizi,
   Nifaulu mitihani, Nipande ngazi kwa ngazi,
   Kaditamati Ahadi, Kadiyaati Mahadi (as).

2. KwaJinalenianzile, Allah MwingiwaRehema,
   Yeyenamuwekambele, Allah MwingiwaKarima,
   KifuaAnitanule, NiyasemeyaHekima,
   KaditamatiAhadi, KadiyaatiMahadi (as).

3. Ahadihiimuhimu, Imo kwenyeKuruani,
   Akharinaminhumu, Ithineniwasitini,
   SuraJumaaAdhimu, wakukadhibishanani,
   KaditamatiAhadi, KadiyaatiMahadi (as).

4. Kumbukawaidhkala, Isa bin Maryama (as),
   Yabanii Siraila, Mtumeyuajanyuma,
   Ahmadiisimila, "Sihiri"wakajasema,
   KaditamatiAhadi, KadiyaatiMahadi (as).

5. Waladhinaamanuu, Waamilasalihati,
   Ukhalifayarjuu, Ni Ahadiilodhati,
   KaahidiAlojuu, Diniiwemadhubuti,
   KaditamatiAhadi, KadiyaatiMahadi (as).

6. Mtukufu Muhammad (saw), AlituasaUmati,
   AkidhihiriMahadi (as), TufanyenayeBayati,
   Lau thelujibaridi, Tumfatehatihati,
   KaditamatiAhadi, KadiyaatiMahadi (as).

7. SifazahuyoMahadi (as), Nazo (saw) alituarifu,
   Imamudhuuweledi, HakimuMuadilifu,
   Firakazitapozidi, YeyetaletaWongofu,
   KaditamatiAhadi, KadiyaatiMahadi (as)

8. Masihitulotajiwa, Kuwa bin Mariyamu (as),
   Ni methalimefumbiwa, Inatakaufahamu,
   Wale wasioelewa, Kelelendioelimu,
   KaditamatiAhadi, KadiyaatiMahadi (as).

9. Yatatokeamaradhi, Kukumbakilabiladi,
   Mdudu toka aridhi, Zama akijaMahadi (as),
   Wadogo na wenye hadhi, Kutubuinatubidi,
   Kadi tamati Ahadi, Kadi yaati Mahadi (as).

10. Tumesikia Munadi (as), Akiita kwa Rabana,
    Sautiye kama Radi, Samiina watwaana,
    Kwa safu na kiweledi, Pa Kitali twapambana,
    Kaditamati Ahadi, Kadi yaati Mahadi (as).

11. Makundi sabi na mbili, Kuluhum fi nnari,
    Ni kauli ya Rasuli (saw), Isilamu tahadhari!,
    Tafakari mara mbili, Sikuta wale ghururi,
    Kaditamati Ahadi, Kadi yaati Mahadi (as).

12. Ndugu zangu wa Ujiji, Wafuata ya mababu,
    Mwenyezi Mungu Ahoji, cha kufata ni Kitabu,
    Kuruani ndio Jaji, si mababu, si warabu,
    Kaditamati Ahadi, Kadi yaati Mahadi (as)

13. Giza limeondokana, Allah nikumsabihi,
    Katupa Nuru bayana, Wenye macho wafurahi,
    Waakhiri daawana, Alhamdulilahi,
    Kadi yaati Mahadi (as), Kadi tamati Ahadi.

Amiri K. Abedi (Msafiri)
Dar es Salaam
22 Machi, 2017

KISWAHILI TUKIPAMBE

Kalamu yangu nishike, na karatasi nirembe
Na kusudi niandike, wimbo kwa watu niimbe
Hapa kwetu usikike, ufike na unyanyembe
Kiswahili tukipambe, kwa mapambo kipambike.

Kwa mapambo, kipambike lugha yetu tuipambe
Tukitaka tuongoke, lugha tusiombeombe
Hii yetu itukuke, tule mfano wa embe
Kiswahili tukipambe, kwa mapambo kipambike

Lazima tukusanyike, kila pembe hadi pembe
Ili tusiaibike, wote harambe harambe
Kiswahili tukisuke, maneno mapya tuchimbe
Kiswahili tukipambe, kwa mapambo kipambike.

Huu ni utamaduni, wa watu waso wazemba
Wa bara na Nisiwani, mfano kufuga ng'ombe
Haya hima wahisani, kama lulu tuilumbe
Kiswahili tukipambe, kwa mapambo kipambike.

Lazima tukikaange, Kiswahili tukiwambe
Sarufi njema tupange, mafumbo ndani tufumbe
Makamusi tuyafunge, ili nasi tujigambe
Kiswahili tukipambe, kwa mapambo kipambike.

Kukipamba kwa kusudi, Songea, Kilwa na Njombe
Tutukuze usanifu, mfano shamba na jembe
Tuipe utundufu, zikomeshwe za wakembe
Kiswahili tukipambe, kwa mapambo kipambike.

Mashairi tahasisu, kila fani tukisombe
Kiwe makali ja kisu, ama kulikoni wembe
Kiswahili tukibusu, kwa ndimi zetu turambe
Kiswahili tukipambe, kwa mapambo kipambike.

Wacheza ngoma wacheze, katika nyimbo waimbe
Na wale wapiga zeze, wa Tunduru kuisombe
Lugha tuitumbuize,kama mnazi iyumbe
Kiswahili tukipambe, kwa mapambo kipambike.

Na tuondoshe ishara, ya busara si uzembe
Kwa kufukuza ujura, misemo ya kikamambe
Kiswahili kiwe bora, na tukilishe kivimbe
Kiswahili tukipambe, kwa mapambo kipambike.

Kiswahili tunukuu, kitu kingine msambe
Waje wetu vitukuu, wa baidi wasichambe
Na tuanze mwaka huu, lugha isiwe mlembe
Kiswahili tukipambe, kwa mapambo kipambike.

Lugha zote za kigeni mapenzi yasitukumbe
Zifukiwe jalalani, si mwenye nyumba za tembe
Kiswahili kuthamini, vichwani mwetu tusombe
Kiswahili tukipambe, kwa mapambo kipambike.

Twawaomba viongozi, leo nawapa ujumbe
Kiswahili kukienzi sio lugha ya upambe
Muondoe pingamizi, ilowekwa na wazembe
Kiswahili tukipambe, kwa mapambo kipambike.

Andanenga
Dar es Salaam

NDEVU

Ndevu unanipendeza, kwa mdomo kuzunguka
Utoto naupoteza, ukubwa umenifika
Ishara ya kujiweza, pirika kuchakarika
Kwa ndevu nimepambika, namshukuru Muweza.

Mithili ya bustani, ndevu zangu ni maua
Zimeota kwa makini, kwa uzuri napumua
Kuna zile za shavuni, pia karibu na pua
Ndevu siha nawambia, namshukuru Manani.

Kwa wembe ukizikata, haziachi uchanua
Uwe kinyozi mtata, lazima zitachipua
Ndugu ndevu ukipata, si vema kuzikwangua
Na kujuza sasa jua, ndevu bahati kupata.

Kwa watu utatajika, yote shauri ya ndevu
Sautiyo kusikika, wetingisha tu kidevu
Uvivu utakutoka, hauwi tena mchovu
Mwenye ndevu yake mbivu, hufurahi malaika.

Raha ya ndevu usafi, ziwe kubwa au ndogo
Hiyo sunna haifi, ndevu katu si mzigo
Ziwe nyeupe za sufi, na nyeusi za kidigo
Ziheshimu si kidogo, mulize bwana hanafi

Ndevu ni thamani kubwa, ukimaizi jamani
Si zamadaru ubwabwa, wazipangao sahani
Kwenye vilio vikubwa, na vidogo bila soni
Kwa kutojua thamani, na akili zikazibwa.

Ndevu huleta thawabu, maarifa na busara
Penye maswali hujibu, ikatoweka hasira
Ndevu pia niwajibu, kwao wajumbe wa shura
Kupata ndevu ni dira, kwa mengi yanayosibu.

Mwisho nina khitimisha, nikingali na ridhiko
Ndevu zangu zanikosha, hupendi shauri yako
Ni Mungu kanirembesha, ndugu ufuge za kwako
Za mwenzako sio zako, unadhani nachekesha?

Mwl. Najat Fakim Said
NANG'OLO = THE BIG BOSS
KINEGEMBASI IRINGA.

BWANA HARUSI

Kwanza nipeni nafasi, kizito nataka juza
Na peaneni nafasi, wala msihofu giza
Nisherehe ya harusi, vinywaji tele agiza
Weka ubani fukiza, yuaja bwana harusi.

Msile kwa wasiwasi, pilau, nyama dabuza
Kuleni pweza na ngisi, na mishikaki ya chaza
Hao punda na farasi, wapandeni mkicheza
Weka ubani fukiza, yuaja bwana harusi.

Mwana mfalme bosi, ndivyo alivyoagiza
Watoto wenye kamasi, sahani zao punguza
Wasije leta mikosi, yai letu liwe viza
Weka ubani fukiza, yuaja bwana harusi.

Tena zidisheni kasi, mapambo pia ongeza
Selemala na patasi, na fundi rangi koleza
Imeni nyimbo za vesi, tena kwa ngoma chagiza
Weka ubani fukiza, yuaja bwana harusi.

Imbeni sisi ni sisi, chongo twaita kengeza
Tumepanga mabalasi, hakuna wakutuweza
Ukiwa kwetu muasi, kweli tunakupoteza
Weka ubani fukiza, yuaja bwana harusi.

Lile jua la utosi, na halijatuunguza
Hatuna cha jumamosi, vibwaya tumevikaza
Uje upepo wa kusi, hatuwezi kulegeza
Weka ubani fukiza, yuaja bwana harusi.

Twatumia karatasi, twaweza kukuduaza
Noti kwetu ni rahisi, kurunzi latuangaza
Sisi wajanja wa kesi, bomu tunaligeuza
Weka ubani fukiza, yuaja bwana harusi.

Sherehe siyo najisi, deka mnavyojiweza
Ni wa kwetu maharusi, nasi wakubwa wa meza
Hakuna wakudadisi, we vimbiwa ukiweza
Weka ubani fukiza, yuaja bwana harusi.

Hii ya mwisho risasi, bunduki naituliza
Japo simba hula nyasi, windo asipokimbiza
Ila nyasi ukakasi, we jipambe bi aziza
Weka ubani fukiza, yuaja bwana harusi.

Mwl. Najat Fakim Said
NANG'OLO = THE BIG BOSS
KINEGEMBASI IRINGA.

UKAME

1. Katikauleukame, niliwezaonamiti
   Ni kushotonakuume, mikono pa samawati
   Kwaduahasazashime, kuiombahasanati
   Mitiiletumaini, seuze we binadamu?

2. Kwaduahasazashime, kuiombahasanati
   Walizoombamitume, tushushiwethamarati
   Na maombindiongome, kutulindanaghalati
   Mitiilitumaini, seuze we binadamu?

Mahmood HamsinMubiruu (Wa Mamba)

Hadhrat Sahibzada Abdul Latif na Ushahidi wake

Na
Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Rabwah, Pakistan.

Sahibzada Seyid Abdul Latif alikuwa mkazi wa Khost, Afghanistan, mtawa mwenye kupokea ufunuo, kashfi na miujiza. Utawa wake uliaminika nchini nzima. Alikuwa na maelfu ya wafuasi katika Afghanistan. Uchamungu, utakaso, elimu na fadhila zake zilikuwa za hali hii kwamba wakati wa kuanza utawala wa Habibullah, Amiri wa Kabul, yeye kwa mikono yake aliweka taji kwenye kichwa chake. Alipenda sana Uislamu na alikuwa akiomba sana kwamba kwa kuhifadhi Uislamu Mwenyezi Mungu Atume haraka Mujadidi mwenye shani kubwa. Katika hali hiyo alipata baadhi ya vitabu vya Hudhur Masihi Mau'udi a.s. Basi kwa kuvisoma safari moja tu alikuwa tayari kujitolea mara elfu, alipata shauku sana kukutana naye. Hatimae alipata mwelekeo moyoni kuenda kuhiji. Hapo alifikiri kwamba njiani atapitia Qadian pia. Alimtajia Amiri wa Kabul pia juu ya nia yake ya hija. Yeye alimruhusu na juu yake alimzawadia fedha kiasi fulani kwa matumizi ya safarini. Kutoka nchini mwake alifika Qadian kwa kukisia katika Oktoba 1902. Kwa kumwona Hudhur a.s. alizama katika mapenzi yake kiasi hiki kwamba muda wa hija ulipita. Aliishi katika Qadian kwa miezi kadhaa.

Kurudi kwake:

Rafiki yake mmoja Mian Ahmad Nur anasimulia kwamba alipokuwa katika Qadian alipata ufunuo huu mara kwa mara kwamba:

"Toa kichwa chako katika njia hii na usijali kwani Mungu Ametaka hivyo kwa heri ya Kabul."

Safari moja alisema kwamba "Nafunuliwa kwamba mbingu inapiga kelele na ardhi inatetemeka kama mtu ambaye ana homa na tikisiko. Dunia inalijua, jambo hili litatokea."

Alipoondoka kutoka Qadian kwa idhini ya Hudhur as, Hudhur a.s. aliungana naye mpaka mbali. Wakati wa kuagana Hadhrat Sahibzada alilia sana na kwa mapenzi makubwa alianguka miguuni ya Hudhur as. Wazee watazamaji wanasimulia kwamba kwa kuona hali yake hiyo hata Hudhur a.s. pia alipata machozi machoni mwake. Hata hivyo hakupenda hii kwamba mtu yeyote amwangukie miguuni mwake au aguse magoti yake kwa heshima. Alimwambia Bwana Sahibzada kusimama lakini yeye alibaki pale pale na vile vile. Hapo alisema kwamba jambo hilo lapita adabu, kwa kusikiliza kauli hiyo mara



Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, aliyewahi kuwa Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahamdiyya nchini Tanzania kwenye miaka ya 1999 - 2001

alisimama na kasema kwamba "Hudhur, sababu ya uzito na huzuni yangu ni hii kwamba moyo wangu una yakini kwamba katika uhai wangu huu sitaweza kukuona tena. Saa hii nakutana nawe mara ya mwisho." Kwa kusema hivi aliaga kwa moyo mzito na macho yenye machozi.

Hadhrat Mian Abdul Aziz Mughal ra, alihadithia mara kadhaa kwamba Hadhrat Sahibzada alikuwa akiweka shuka juu ya kilemba chake na alikuwa akivaa kanzu kubwa. Katika muda wa kukaa Lahore mtu fulani aliwakaribisha ndugu wachache kwenye hafla fulani. Humo Hadhrat Sahibzada pia alienda. Bwana Mughal alikuwa akisema kwamba katika karamu ile mimi pia nilienda kwa Hadhrat Sahibzada. Alipofika kwenye chumba cha karamu humo vyakula vya aina aina vilipangwa mezani kwa njia nzuri sana. Hadhrat Sahibzada alipoketi tu alipata hali ya kashfi na aliniambia katika lugha ya Kifarsi kwamba mmenileta hapa kwa kunilisha haramu. Alisema hivi na kasimama na alianza kutembea haraka haraka, na kanzu yake ilipepeteka hewani. Njiani alinipa Anna nne na kasema kwamba nunua chapati na kebabu, nilifuata amri. Chapati na kebabu zilizokuwa nyingi, tulikula tukikaa katika msikiti Gumti wali, siku hizi ulio chini ya usimamizi wa Jumuiya Ahmadiyya. Mwenyeji alipomwona Hadhrat Sahibzada akirudi basi aliathirika sana na jicho lake la kashfi kwani alijua kwamba karamu hiyo ni ya fedha ya riba.

Akitoka Lahore alienda kwake Khost. Njiani aliwaambia wanafunzi wake mara kwa mara kwamba ardhi ya Kabul inahitaji damu yangu kwa urekebisho wake. Kwa vile hali za baadae Hudhur a.s. mwenyewe ameandika katika kitabu chake Tadhkiratush Shahadatain, kwa hiyo zile zinaelezwa kimuhtasari kwa maneno ya Hudhur a.s. tu.

Ushahidi wa Hadhrat Sahibzada Abdul Latif
14 Julai 1903:

Alipofika karibu na jimbo la Kabul, akikaa katika eneo la serekali ya Kiingereza alimwandikia barua Brigadier Muhammad Husain mkuu wa polisi, aliyekuwa mwanafunzi wake kwamba niombee ruhusa kutoka Amiri kisha niarifu ndipo nimwendee Bwana Amiri huko Kabul. Hakuenda bila kuomba ruhusa kwa sababu wakati wa kuenda safarini alimwambia Amiri kwamba anaenda kuhiji lakini hakuweza kutimiliza nia ile kwa kukaa sana katika Qadian na wakati ulipita … Basi aliona vizuri kwamba amwandikie Brigadier Muhammad Husain ili kwa wakati mwafaka na maneno mazuri amwambie Amiri. Alimwandikia katika barua hiyo kwamba ingawa nilitoka kwa nia ya kuhiji lakini nilipata kuonana na Masihi Mau'udi. Na kwa vile kwa kumwona Masihi na kwa kutanguliza utii wake kuna amri ya Allah na Mtume s.a.w. , kwa ulazima huo nililazimika kukaa Qadian. Na sikufanya hivi kwa ridhaa yangu bali sawa na Qurani na Hadithi jambo hilo niliona muhimu. Barua hiyo ilipomfikia Brigadier Muhammad Husain basi aliiweka chini ya goti yake na hakupeleka wakati huo. Lakini makamu wake aliyekuwa mpinzani na mwenye shari alijua kwa njia yoyote kwamba hiyo ni barua ya Sahibzada Abdul Latif na alikaa katika Qadian ndipo alichukua barua ile kwa ujanja fulani na aliimpelekea Amiri … Kwa vile ushahidi wa Bwana Sahibzada ulipangwa kwa kadhaa na mbinguni alikwishaingia katika kundi la mashahidi walioteuliwa. Kwa hiyo Bwana Amiri alitumia ujanja kwa kumwita na alimwandikia kutoka kwa Brigadier kwamba uje bila wasiwasi wowote. Kama madai hayo yatakuwa kweli basi mimi pia nitakuwa mfuasi … Wasimulizi wanasimulia kwamba Shahidi Marehemu alipopita sokoni Kabul, alipanda farasi na nyuma yake walikuwepo wapandaji nane wa farasi wa serekali … Na walisimulia hii pia kwamba hao wapandaji nane wa farasi wa serekali walimfuatilia kutoka Khost. Kwani kabla ya kufika kwake Khost amri ya serikali ya kumkamata ilitolewa kwa jina la Hakimu wa Khost. Ilimuradi alipoletwa mbele ya Amiri, wapinzani tayari walimkasirisha sana, kwa hiyo alimpokea kwa njia ya dhuluma sana na aliamuru kwamba napata hurufu mbaya kutoka kwake, mwekeni mbali. Kisha baada ya muda mfupi aliamuru kwamba mfungeni katika ngome ile anapoishi Amiri mwenyewe na afungwe minyororo ya Gharagharab. Mnyororo ule una uzito wa kilo 64 ya kiingereza, unaozunguka kuanzia shingo mpaka kiuno na inakuwepo pingu pia pale pale. Vile vile aliamuru kwamba mnyororo wa pili wa kilo nane ya kiingereza ufungwe miguuni. Katika hali hiyo Bwana Sahibzada Marehemu alibaki gerezani kwa miezi minne. Katika muda huo mara kadhaa alimwambia kwamba kama ukitubu na mawazo haya kwamba Bwana Qadiani yu Masihi Mau'udi basi utaachwa. Lakini kila mara alimjibu hivi kwamba mimi ni mwanachuoni, Mungu Amenijaalia uwezo wa kutambua haki na batili, nimeshagundua kwa utafiti kamili kwamba kwa kweli mtu huyo ni Masihi Mau'udi. Ingawa najua kwamba kwa kufuatilia njia hiyo uhai wangu hauna usalama na familia yangu itaangamia lakini wakati huu natanguliza imani yangu juu ya uhai wangu na juu ya kila raha ya dunia … Miezi minne ya gerezani ilipopita Bwana Amiri akimwita Shahidi Marehemu mbele yake, alimwomba kutubu. Na alimhimiza sana kwamba hata sasa pia ukikana mbele yangu usadikishaji wa Bwana Qadiani na usadikishaji wa itikadi zake basi nitakusamehe uhai wako na utaachwa kwa heshima. Shahidi Marehemu alijibu kwamba hiyo haiyumkiniki kwamba nitubu na niache ukweli. Adhabu ya watawala wa dunia hii itakwisha kwa mauti lakini namwogopa Yule ambaye adhabu yake haiwezi kuisha kamwe. Naam, kwa vile miye mkweli, kwa hiyo nataka kwamba upangwe mjadala wangu na masheikh walio wapinzani wa itikadi yangu. Nikikutwa mwongo kwa hoja basi niadhibiwe … Amiri alipendekeza jambo hilo na katika Masjid Shahi, Khan Mulla Khan na mamufti nane walichaguliwa kwa mjadala. Daktari mmoja aliyekuwa mpinzani mkali kwa kuwa wa Panjab alitumwa kuwa jaji. Wakati wa mjadala ilikuwepo halaiki kubwa. Watazamaji wanasimulia kwamba tulikuwepo katika mjadala, mjadala ulikuwa kwa kimaandishi, yalikuwepo maandishi tu na wasikilizaji hawakusomewa jambo lolote. Kwa hiyo haikujulikana hali yoyote ya mjadala. Kuanzia saa moja asubuhi mpaka saa tisa Alasiri mjadala uliendelea. Kisha mwisho wa wakati wa Alasiri alipewa fatwa ya kufuru. Na mwisho wa mjadala Shahidi Marehemu aliulizwa hii pia kwamba kama huyo Bwana Qadiani ndiye Masihi Mau'udi basi usemaje juu ya Isa a.s., je, atarudi duniani au la? Hapo alijibu kwa uimara sana kwamba Hadhrat Isa a.s. ameshafariki, sasa hatarudi kamwe. Qurani Tukufu ni shahidi juu ya kufa na kutorudi kwake. Ndipo watu hao, sawa na masheikh ambao walipasua nguo zao wakisikiliza kauli ya Hadhrat Isa a.s., walianza kutusi na wakasema kwamba haikubaki shaka yoyote katika kufuru ya mtu huyu na katika hali ya ghadhabu sana fatwa ile ya kufuru iliandikwa … Kisha baada yake wakati wa usiku fatwa hiyo ya kufuru ilipelekwa kwa Bwana Amiri na walifanya ujanja huu kwamba hawakumtumia kwa kusudi karatasi za mjadala wala watu wa kawaida hawakudhihiri-shiwa madhumuni yake. Hiyo ilikuwa dalili wazi wazi ya jambo hili kwamba masheikh wapinzani hawakuweza kujibu hoja zilizoletwa na Shahidi Marehemu. Lakini masikitiko juu ya Amiri kwamba aliamuru juu ya fatwa ya kufuru na hakuomba karatasi za mjadala … Shahidi Marehemu alipokana kutubu kila mara alipoombwa kutubu ndipo Amiri akikata tamaa, aliandika karatasi kubwa kwa mkono wake na humo aliandika fatwa ya masheikh na humo aliandika hii pia kwamba adhabu ya kafiri wa aina hiyo ni kupiga mawe, ndipo fatwa ile iliwekwa shingoni mwa Sahibzada

Endelea uk. 9

Mbashiri wa kwanza Mzalendo wa kujitolea Afariki

Na Al-Ustadh Khamisi Sultan S. Wamwera – Dar es Salaam

Kutoka toleo lililopita

WATU WANAJIUNGA NA AHMADIYYA

Sheikh Abdulkarim Sharma karibu siku tatu akishirikiana na Sheikh Swaleh waliwaweka watu sawasawa. Khatimae Sheikh Sharma aliwaambia wana kijiji cha Nyipara na wa pembezoni mwake umuhimu wa kujiunga katika Jumuiyya ya Ahmadiyya. Siku ile watu 150 walifanya Baiat bila kushurutishwa. Sheikh Sharma aliporejea Dar es Salaam alirudi na rundo la Baiat. Neema kubwa kabisa.

SASA NYIPARA YA AHMADIYYA

Sasa kijiji cha Nyipara ni cha Jumuiyya kwa sababu zaidi ya robo tatu ya wakazi wake wameshajiunga katika Ahmadiyya. Ukiachia neema ile ya mahindi, simsim na mpunga, miembe, migomba na mipapai, mabwawa na hili la kuwa katika kundi la Masihi Aliyeahidiwa ni neema nyingine iliyo kubwa kuliko.

Watu wa janibu zingine walipiga kelele na mayowe kwamba Nyipara imezama katika upotevu na kufuru. Wenyeji wake wamepotezwa na hivyo wametanasari na kuritadi. Wale Masheikh niliowataja hapo juu baada ya kushindwa kujitokeza mbele ya Ahmadiyya kwa mjadala, wakaanza kutia sumu kwenye mtazamo wa watu ambao bado wana mapenzi na Jumuiyya. Walileta maneno mengi ya chuki na hiyana. Waliwaambia watu kuwa Waahmadiyya wanapigwa mihuri matakoni na kwamba wale wanaojiunga katika Ahmadiyya wanapewa fedha! Ndipo walipotowa fatuwa ya kwamba yeyote aliyejiunga na Ahmadiyya si Islam. Wakawaamrisha wafuasi wao, hususan wale walioozesha mabinti wao kwa hawa waliojiunga katika Ahmadiyya hivi sasa mara moja wanyang'anywe na hakuna eda yoyote. Kama mwanamume atapatikana leo, basi ndowa inaweza kufanyika kwa mwanamume mwingine.

MTIHANI MKUBWA

Wanajumuiyya wengi walinyang'anywa wake wao. Kwa kweli huu ulikuwa mtihani mkubwa. Ni tukio ambalo lilitikisa imani ya watu na kuwaimarisha wengine. Hapa hebu niwataje akina mama wawili ambao kwa hakika walisimama imara kutetea imani yao. Wa kwanza ni Bi. Mariyamu binti Muhammad Mpapu ambaye alikuwa mke wa Mzee Maliki Abdullah Mbungiro (Watachoka) na wa pili mke wa Bwana Jafari Aliy



Al-Ustadh Khamisi Sultan S. Wamwera



Al Marhuum Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima

Nyamkwasu. Akina mama hawa wawili walipofikiwa na wazazi wao na kuwataka waondoke kwa waume wao, hawa mabinti hawakukubali. Bi. Mariyamu alikosewa radhi na wazazi wake kwa kutotii vile walivyokuwa wanataka wao. Mke wa Bwana Jafari pia palikuwa mambo. Wazazi wa huyu binti walifika kwa Bwana Jafari na fedha zao mkononi na kumwambia binti yao aondoke kwa mumewe nao wanarejesha fedha ambazo zilitolewa hapo mwanzo kama mahari. Huyu binti aliwajibu wazazi wake kuwa yeye haendi popote bali atabaki kwa mumewe. Juu ya fedha, alisema hiyo apewe kwa sababu wazee walizichukua bila kujuwa mahari ni haki ya nani. Mahari ni haki ya muolewaji si mzazi. Ninamuomba Mwalimu Mahmood Hamsin Mubiru ambaye ni mwanahistoria wetu asiwasahau akina mama hawa wawili ambao wameonesha ukakamavu mkubwa katika imani. Haya ni matunda khalisi ya kazi ya Sheikh Swaleh Mbaruku.

Ngoja nieleze kisa kingine cha ajabu sana, lakini ndani limo somo la imani na elimu yakini. Mwalimu Omari Abdullah Matimbwa alijiiunga katika Jumuiyya bado kijana sana, mnano mwaka 1956. Babaye alichachamaa kweli kweli. Alikasirika na kununa. Huyu mzee alikuwa anaishi kijiji cha pili akapata habari mwanaye amejiunga na Ahmadiyya. Siku moja alifika Nyipara ili amchukue mwanawe kwa nguvu. Mwalimu Omari alibebwa juu kwa juu huku akicharazwa bakora. Alitupwa chini kama gunia la viazi mbatata. Aliburuzwa chini kama kitu kichafu. Mwalimu Omar alipoulizwa ataacha Ahmadiyya na amfuate babaye, alimwambia baba yake kwamba anachoweza kukiharibu ni kiwiliwili chake, lakini hawezi kubadili imani yake kwa njia aliyopitia baba yake. Mwalimu Omari Abdullah Matimbwa akang'ang'ania katika imani yake katika Jumuiyya ya Ahmadiyya.

MAMBO MAHAKAMANI

Uadui ulikithiri mno, usalama na amani ilikuwa haba. Serikali ikaelezwa hali hiyo. Mashauri yakapelekwa Mahakamani. Ni katika miaka ya 1957/58. Waahmadiyya walidai kuwa Masheikh wa Kisuni walikuwa wanawachochea wazazi wa mabinti waliozawijiwa na Waahmadiyya wanyang'anywe hao wanawake kwa sababu ati ya kubadili dini. Mahakama ikapokea shauri hili. Wahusika waliitwa na mahakama kujibu tuhuma hiyo. Sasa hapa mahakamani, huku kuna Sunni na wafuasi wao na huku kuna Wanajumuiyya ya Ahmadiyya wakiongozwa na Maulana Sheikh Amri Abedi. Ni siku ya kusikilizwa tatizo lililojitokeza. Kwa kweli siku hiyo mahakamani hapo palifurika watu waliofika kusikiliza shauri hili. Masuni walifika mahakamani hapo hoi hoi kwa dhikri ya Abdul Qadir Jailani huku wakisema leo ni leo. Mahakama ilianza kupokea maelezo kutoka kwa Sheikh wa Sunni aliyejaribu kuieleza Mahakama hiyo ukafiri wa Ahmadiyya. Alisema ukafiri wa Ahmadiyya ni kule kuamini mtume mwingine, baada ya Mtume wetu Muhammad (saw). Pia hawa hawaamini Nabii Isa amepaa na atarejea hapa duniani tena. Matanga na tarakini, wanasema si mafundisho ya Islam. Kwa imani kama hii moja kwa moja mtu anakuwa nje ya Uislamu.

Upande wa Ahmadiyya akasimama Maulana Sheikh Kaluta Amri Abedi kujibu tuhuma zote zilizotolewa na Sheikh wa Kisunni. Moja baada ya moja. Sheikh Amri aliiambia Mahakama ambayo Hakimu aliyekuwa anasikiliza mashauri haya alikuwa Msuni kwamba Ahmadiyya si dini mpya na yale yote yanayoelezwa ni mafundisho ya Qur'an Tukufu wala hayatoki kwenye kitabu kipya. Ama kuendelea kwa utume si neno lililozushwa na Ahmadiyya, bali hii ni neema ya Allah ambayo hwaja wake wakati wote. Na kama tunaamini Nabii Isa kapaa mbinguni, na Nabii wetu mtukufu Muhammad (saw) amekufa na kuzikwa kwenye matope haya ya ardhini, ni nini na upo wapi ubora wa mtukufu Mtume Muhammad Mustafa (saw)? Ni wazi, Sheikh Amri aliiambia Mahakama; "Ahmadiyya ni Jumuiyya inayosimamia mafundisho safi ya Kiislamu yaliyoachwa na watu wengi hivi sasa". Bwana Hakimu hatua iliyochochewa na Masheikh hawa ya kunyang'anya Waahmadiyya wake wao kwa sababu ati si Waislamu, haina m singi hata kidogo. Si hatua sahihi bali hiyo ni fujo na unyanyasaji. Maulana K. Amri Abedi alimweleza Hakimu kwamba kama si subira na uvumilivu waliouonesha Waahmadiyya kutoka katika mafundisho ya Uislamu, ghasiya na fujo kubwa ingetokea na usalama ungetoweka. Lakini Ahmadiyya wanaongozwa na Qur'an Tukufu, hayo hayakutokea.

HAKIMU ATOA HUKUMU

Hakimu ambaye jina lake alikuwa Saidi Mohammad Matendekeya baada ya kuokea maelezo ya pande zote mbili na kuyachambua kwa makini. Alitoa hukumu ifuatayo; "Mwana Nunu aliyeolewa kisheria, mzazi, mlezi au mtu mwingine yeyote , kamwe hawezi kuvunja ndoa ya bintiye vyovyote iwavyo. Ni mume na mke tu hawa wawili ndiyo wenye jukumu la kudumisha nikaha yao au kuivunja. Pili, ni Mahakama tu inaweza kuchukuwa hatuwa ya namna hiyo pawapo madai ya kweli kutoka mmoja wapo kati ya mume na mke". Hakimu akaendelea kusema kwamba kitendo kilichofanywa na wazazi hawa kwa kuwanyang'anya Waahmadiyya wake wao baada ya kushawishiwa na masheikh wao si kitendo cha halali. Ni kosa wala si haki. Kuanzia sasa binti yeyote aliyetolewa kwa mumewe, arejeshwe kwa mumewe mara moja".

KULITOKEA KITU GANI?

Mahakama baada ya kutowa hukumu hiyo, Wasuni wote waliokuwa pale walishangazwa sana hasa wakiamini Hakimu alikuwa mwenzao. Walinyanyua sauti zao na kumwambia Hakimu ati amewapendelea Ahmadiyya. Walinywea kweli kweli, walikuja mahakamani na bendera ya dhikri na hoihoi nyingi, sasa wanaondoka pale kimya kimya kila mmoja na njia yake. Hawakuwa na habari hata na Yule Sheikh wao! Allahu Akbar.

Baada ya tukio hili, Nyipara na Jumuiyya ya Ahmadiyya ekaenea Rufiji yote. Kila aliyekaa hapo japokuwa si Mwanajumuiyya, lakini alijulikana kama Mwanajumuiyya. Watu wa Nyipara walimshukuru mno Mwenyezi Mungu kwa fadhila na neema kubwa waliyopata kwa ujio wa Sheikh Swaleh Mbaruku. Waliona Baraka kubwa sana kumpokea Masihi na Mahadi ambaye kwa hakika tuliambiwa tutambae hata kwenye theluji ili tumfikie aliko, lakini wao wameletewea pale pale Nyipara. Jumuiyya ya Ahmadiyya Nyipara ikawa imeimarika sawasawa. Kila mmoja alikuwa anaogopwa kwa masaala ya dini.

Sheikh Swaleh Mbaruku alipoona mambo si mabaya akawa na mawazo ya kwenda Njinjo Kilwa kumchukua mkewe na wanawe. Wazo hili aliliwakilisha mbele ya waumini, lakini halikupata nafasi ya kulipitisha. Walikuja juu na kumweleza Sheikh kwa wakait ule asiwe na wazo hilo, bali aendelee kusubiri hadi hapo baadae. Kama kawaida Sheikh Swaleh alitumia hekima, ndipo akamwandikia barua Maulana Sheikh Mubarak Ahmad wakati huo ndiye alikuwa Mbashiri Mkuu Afrika Mashariki. Alimweleza dhamira aliyonayo ya kwenda Kilwa kuchukua watoto wake. Maulana Sheikh Mubaraka naye alimkatalia, bali alimwambia aendelee kubaki Rufiji kuwalea Wanajumuiyya waliopo pale. Kwa heshima na taadhima Sheikh Swaleh alimwandikia tena Sheikh Mubaraka huku akimkumbusha ile aya inayomtaka Mtume Mtukufu Muhammad (saw) awafikishie kwanza ujumbe wale ndugu zake wa karibu. Kwa maelezo hayo, Sheikh akapewa ruhusa ya kwenda Kilwa.

NYUMBANI KILWA

Sheikh Swaleh Mbaruku baada ya kukaa Rufiji miaka mitatu sasa anafika kwenye ardhi ya kwao Njinjo Kilwa na kukutana na ahali wake, ndugu na majirani wake. Watoto wanafurahi kumuona mzazi wao, mama anafurahi kumuona mumewe. Furaha moja kwa moja.

DARASA LAFUNGULIWA

Kwake Sheikh Swaleh ilikuwa hakuna kulala. Uzoefu alioupata pale Nyipara Rufiji ilitosha yeye kuendelea mbele. Kama vile Rufiji, Sheikh Swaleh akatumia mbinu ile ile. Akafungua darasa Njinjo, wanaotaka elimu wakaja kwa wingi. Huyu Fiqhi, huyu taratibu swalat, n.k Darasa likastawi kwa watu. Akaanza kutowa tafsiri ya Qur'an Tukufu ambapo zamani ilikuwa vigumu elimu yake kupatikana. Hili lilichukua watu wengi kulipenda. Wengi walisongea karibu ya Sheikh kujichotea elimu. Sheikh Swaleh kama kawaida yake, alienda taratibu na watu hao, wala hakuwa na papara na haraka. Kwanza alitaka wanafunzi wake wamkubali. Alitaka tirmidhi wake wakomae kwa yale aliyolenga kuwafundisha. Mungu bariki siku ikafika mambo yakawa jahara.

Itaendelea toleo Lijalo. Inshallah

-

Hadhrat Sahibzada Abdul Latif na Ushahidi wake

Kutoka uk. 7

Marehemu. Kisha Amiri aliamuru kwamba Marehemu akidungwa puani na humo atiwe kamba, na akivutwa na kamba hiyo hiyo afikishwe mpaka mahali pa kuuawa yaani mahali pa kupigwa mawe. Basi kwa amri ya Amiri mdhalimu ikafanywa hivyo, pua ilidungwa na kamba ikatiwa kwa adhabu kali sana. Kisha kwa kamba hiyo hiyo akivutwa kwa mzaha, kuchekwa, matusi na laana alipelekwa kwenya mahali pa kuuawa. Na Amiri kwa masahibu wake, makadhi, mamufti na maafisa wengine akitazama nadhara hiyo ya mateso alifika mpaka mahali pa kuuawa. Na halaiki kubwa ya maelfu ya mji isiyohesabika, ilienda kuona tamasha hiyo. Walipofika kwenye mahali pa kuuawa Bwana Sahibzada alizikwa ardhini mpaka kiunoni. Kisha katika hali hiyo alipozikwa ardhini mpaka kiunoni Amiri alimfikia na kasema kwamba ukimkana Bwana Mirza anayedai kuwa Masihi Mau'udi, hata sasa pia nitakutunza, sasa ni wakati wako wa mwisho na hii ni nafasi ya mwisho unayopewa, ujihurumie na familia yako. Hapo Shahidi Marehemu alijibu kwamba Mungu apishe mbali, kutakuaje kukana ukweli, Na uhai una uzito upi, familia na watoto ni kitu gani ambao kwao niache imani, sitafanya hivi kamwe bali nitakufa kwa haki. Ndipo Makadhi na mamufti walipiga makelele kwamba ni kafiri, ni kafiri, mpigeni mawe haraka. Wakati ule Amiri na kaka yake Nasrullah Khan, Kadhi na Abdul Ahad Komidan walipanda na watu wengine wote walikuwa kwa miguu. Katika hali hiyo kali Shahidi Marehemu mara kwa mara aliposema kwamba ninatanguliza imani juu ya uhai ndipo Amiri alimwamuru kadhi kwamba piga wewe jiwe la kwanza kwani umetoa fatwa ya kufuru. Kadhi alijibu kwamba u mfalme wa zama hizi, upige wewe. Hapo Amiri alijibu kwamba wewe ndiwe mfalme wa sheria na fatwa pia ni yako, humo sina mamlaka yoyote. Ndipo Kadhi akishuka farasi alipiga jiwe ambayo kwayo Shahidi Marehemu alipata jeraha kali na shingo liliinama. Kisha baada yake Amiri, mwenye bahati ndogo, alipiga jiwe kwa mkono wake, hapo kwa kumfuata maelfu ya mawe yalirushwa kwa Shahidi. Na hakuwa yeyote kati ya wahudhuriao ambaye hakumpiga Shahidi. Kiasi hiki kwamba kwa mawe mengi rundo kubwa la mawe likajumuika juu ya kichwa cha Shahidi Marehemu. Kisha wakati wa kurudi Amiri alisema kwamba mtu huyu alisema kuwa katika siku sita nitafufuka, kwa hiyo ulinzi uwekwe kwa siku sita. Imesimuliwa kwamba dhuluma hiyo yaani kupiga mawe ilitokea tarehe 14 Julai 1903 … Ushahidi uliopangwa kwa Shahzada Abdul Latif ulitendeka, Sasa adhabu kwa mdhalimu imebaki … Ee Abdul Latif, maelfu za rehema ziwe juu yako, kwamba umeshaonyesha mfano wa ukweli wako katika uhai wangu tu na watu wa Jumuiya yangu ambao watabaki baada ya kifo changu, sijui kwamba watafanya nini."

Hudhur a.s. akieleza hali zilizobaki za Bwana Shahidi ameandika mwishoni mwa kitabu chake "Tadhkiratush Shahadatain":

"Mian Ahmad Nur aliye mwanafunzi maalum wa Hadhrat Sahibzada Maulawii Abdul Latif, leo tarehe 8 Novemba 1903 amefika Qadian kutoka Khost kwa familia. Anasimulia kwamba mwili wa Shahidi ulibaki kwa siku arobaini katika mawe aliyopigwa. Baada yake mimi na ndugu wachache wakati wa usiku tulitoa mwili na kwa siri tukauleta mjini. Ilihofiwa kwamba Amiri na wafanyakazi wake watazuia lakini kwa sababu ya kuenea kwa kipindupindu mjini, kila mtu alikuwa na mahangaiko yake. Kwa hiyo, kwa utulivu tu tulepeleka mwili wake makaburini, tukisali sala ya jeneza humo tulimzika. Hii ni jambo la ajabu kwamba Bwana Shahidi alipotolewa kutoka maweni manukato aina ya miski yalitoka kutoka mwili wake, watu waliathirika sana na hiyo."

Matokeo ya uuaji huo usio na haki:

Hudhur a.s. ameandika katika kitabu chake hicho "Tadhkiratush Shahadatain" kwamba

"Ardhi ya Kabul itaona kwamba uuaji huo utazaa tunda la aina aina. Uuaji huo hautapotea kamwe. Kabla yake Abdur Rahman wa Jumuiya yangu aliuawa kwa dhuluma na Mungu Alinyamaza lakini kwa uuaji huo sasa hatanyamaza na matokeo makubwa makubwa yatadhihirika. Basi imesikika kwamba Shahidi Marehemu alipouawa kwa maelfu yamawe, siku zile kipindupindu kikali kilienea katika Kabul na wakubwa wengi walishikwa nacho na baadhi ya jamaa wa Amiri pia waliaga dunia lakini hiyo si kitu. Uuaji huo umefanywa kwa dhuluma sana na katika zama hizi chini ya mbingu hautapatikana mfano wa uuaji wa namna hiyo. Amefanya nini huyo Amiri mjinga kwani amejiangamiza kwa kumwua mtu wa aina hii asiye na kosa kwa dhuluma kubwa sana. Ee Ardhi ya Kabul, uwe shahidi kwamba kosa kubwa limefanyika juu yako. Ee ardhi yenye bahati ndogo, umeshaanguka katika macho ya Mungu kwani u nchi ya dhuluma hiyo kubwa."

Katika uuaji huo kuliko Amiri wa Kabul alihusika zaidi kaka yake Sardar Nasrullah Khan. Bwana Angus Hamilton anaandika juu ya hali hiyo:

(Siku ya pili ya kuuawa kwa kupigwa mawe yaani tarehe 15 Julai 1903.) "Katika mji wa Kabul wa Afghanistan na mikoa yake ya kaskazini na mashariki kipindupindu kilienea sana kilichokuwa kibaya zaidi kuliko maradhi ya kipindupindu ya 1879. Mke wa Sardar Nasrullah Khan, mvulana wake na watu kadhaa wa familia ya kifalme na maelfu ya wakazi wa Kabul walikufa kwa maradhi hiyo. Machafuko yalitokea mjini kwani kila mtu alilazimika kujijali na alisahau kabisa hali za wengine."

Uuaji wa Amiri Habibullah Khan – 20 Februari 1919:

Amiri Habibullah Khan ambaye katika utawala wake Hadhrat Shahidi Marehemu aliuawa kwa kupigwa mawe, kwa ujanja wa kaka yake tarehe 20 Februari 1919 wakati wa kulala usiku aliuawa kwa risasi moja tu la bistoli.

Mwisho wa Sardar Nasrulla Khan:

Baada ya kuuawa kwa Amiri Habibullah Khan, Sardar Nasrullah Khan alijifanya mfalme akinyag'anya haki ya mrithi wa kweli Sardar Anaitullah Khan. Kuona hali hiyo Sardar Amanullah Khan aliyekuwa mwana wa tatu wa Amiri Habibullah Khan akiungana na kamati ya utawala na masheikh alishikilia utawala kwa nguvu na aliamuru kuwahudhurisha Sardar Nasrulla Khan na wenzake wakifungwa minyororo miguuni. Tarehe 2 Aprili 1919 alifungwa katika jela ya kifalme na baadae waliwekwa katika mnara fulani. Inasemekana kwamba kwa huzuni hiyo akawa mwendawazimu. Baada ya muda fulani aliuawa akifungwa pumzi. Hii pia inesemekana kwamba daktari Ahmad Beg Mturuki msaidizi wa daktari Munir Izzat alimwua mwishoni mwa Aprili 1919 kwa kumlisha sumu kwa amri ya Amiri Amanullah Khan.

Mwisho wa Abdul Ghani, Daktari wa Panjab:

Daktari Abdul Ghani, "Daktari wa Panjab" aliyekuwa jaji katika hafla ya mjadala kwa ndugu zake alifungwa kwa miaka kumi na moja. Mke wake alipotaka kuja Panjab kutoka Kabul basi njiani kwenye sarai ya Landikotal alifariki na watu walikusanya fedha kwa sanda na kuzika. Kijana wake Abdul Jabar alikuwa anarudi kuleta vitu kutoka sokoni. Yeyote alitoa kichwa chake akimpiga upanga kutoka nyuma.

Mwisho wa Sheikh Abdur Razak, Kadhi:

Sheikh Abdur Razak, Kadhi aliyempigia Shahidi Marehemu jiwe la kwanza kabisa, hali yake ilikuwa hii kwamba Amiri wa Kabuli Habibullah Khan alitoa amri hii kwamba mtu yeyote asitembee barabara yoyote upande wa kulia bali watu wote watembee upande wa kushoto. Siku moja Amiri wa Kabul alipita barabarani, aliona kwamba Sheikh Abdur Razak Khan, Kadhi Mkuu anatembea barabarani upande wa kulia na polisi aliye kazini anamkataza lakini yeye hamuitikii. Amiri wa Kabul akiona hiyo alimfaini rupia 1000. Baadae katika zama za Amiri Amanullah Khan aliamrisha kumpiga mijeledi na kuhudhuria kila siku kama mshtakiwa. Baada ya adhabu hiyo alipotea kutoka Kabul kana kwamba alijizika mzima.

Familia ya Amiri Habibullah Khan ilikosa utawala:

Mwenyezi Mungu Angetaka angenyang'anya utawala kutoka familia ya Amiri Habibullah Khan wakati uleule lakini aliwapa muda fulani ili familia hiyo ijirekebishe. Lakini familia hiyo haikuweza kutenda mema wowote basi mtu wa kawaida sana, Bacha Saka aliwafukuza kutoka nchini akimshambulia Amanullah Khan, Amiri wa mwisho wa familia hiyo.

(Kutoka Maisha Matakatifu ya Seyidna Ahmad a.s.)

Dhambi zimetamalaki dunia kuliko matendo mema?

Na Ayoub SADI- Dar Es Salaam.

Wiki moja iliyopita, nilikuwa nazungumza na mmoja wa rafiki zangu kwa njia ya ujumbe wa kawaida katika simu yangu ya mkononi. Katika mazungumzo yale, yule rafiki yangu ambaye mpaka sasa tungali tunafanya kazi za kujiongezea ujuzi katika studio za kituo cha Runinga na Redio cha Mlimani ambacho kinasimamiwa na kumilikiwa na Chuo Kikuu cha Dar es salaam, aliniambia kuwa siku hizi dhambi zimeongezeka na shetani amekithiri. Kwa kuwa tulikuwa katika mazungumzo ya kawaida, sikutarajia kusikia ile kauli kutoka kwake. Pengine alivutiwa na muktadha wa mazungumzo yale.

Swali hilo nikaliuliza kwa watu zaidi ya 10 na nikapokea majibu yanayofanana. Wote walijibu kuwa Dhambi zimeongezeka au kuzidi duniani na matendo mema au yenye kustahili thawabu yamepungua au ni ya nadra sana katika ulimwengu wa sasa. Kwa ufupi, dhambi ni nyingi duniani kuliko mema.

Tukichunguza kwa umakini sana utaona majibu yaliyotolewa dhidi ya swali lililoulizwa hayana uhalisia katika mazingira halisi ya mwanadamu iwe katika zama zilizopita au zama tulizopo hivi sasa. Islam inafundisha kwamba mwanadamu kwa asili, amezaliwa akiwa na silka au tabia halisi za kutokuwa na dhambi, lakini ni wazazi wake ndio wanaoamua awe mtu mwema ama muasi. Kwa kuzingatia hilo, hebu tuangalie ni kwa namna gani mtu anaweza kupima matendo mema au dhambi katika jamii na dunia kwa ujumla.

Uwepo wa matukio yenye sura za mauaji ya kutisha, kukithiri kwa vitendo vya kigaidi, vitendo vya ubakaji, utekaji nyara ni mojawapo ya matendo yasiyofaa au dhambi ambayo yamekuwa yakifanyika kila kukicha katika uso wa ardhi. Vitendo vya wizi, utapeli, usengenyaji, na hata uzinzi ambao kwa hivi sasa umekuwa bidhaa rahisi na kufikia kupigiwa upatu hata na wana siasa katika kampeni zao, yamekuwa yakiendelea kushamiri na kumtisha mwanadamu ambaye hupenda heri na kuchukia shari na maasi ya aina hiyo ambayo huvutia ghadhabu na adhabu za Mungu duniani. Wingi wa matendo hayo humfanya mwanadamu yule anayeyatazama hayo kwa jicho la nje au juu juu tu kudhani kwamba kipimo chake kuhusu dhambi na mema huenda kikawa kimefikia ukomo na kuipa hatamu dhambi mbele ya wema. Bila shaka, kwa mtazamo huo, inayumkinika kuamini kuwa dhambi zimetamalaki duniani kuliko mema.

Hebu tuchunguze kwa umakini. Mwanadamu hutazama na kuyaweka katika vitendo vya dhambi mambo kama wizi, uzinzi, unyanganyi, uuaji, usengenyaji, kutazama wanawake, kutukana, kufanya ufisadi, ugaidi na n.k. Lakini tukivitazama vitendo hivi kwa undani, tunaona kuwa kwa wale wanaovifanya au kuvishiriki hawafanyi hivyo siku nzima ya maisha yao. Kwa mfano muuaji. Huenda akafanikiwa kutoa roho za wanadamu wenzake nyingi tu kwa siku, lakini mtu huyu hawezi kufanya jambo lenyewe siku nzima. Hawezi kulifanya tendo la uuaji likawa ndio shughuli yake ndani ya masaa 24 yanayokamilisha siku moja. Ni lazima mtu huyu atapumzika na kufanya shughuli nyingine iwe kula, kunywa, kulala au kuongea na watu n.k. Mwanadamu kwa kawaida hutumia masaa 6 au 8 kwa ajili ya kulala na kuupumzisha mwili wake.

Katika moja ya hotuba zake za Jalsa Salana, Khalifa wa Pili Hadhrat Mirza Bashirud Din Mahmood Ahmad r.a alipata kujibu swali kutoka kwa mmoja wa waliouhudhiria katika mkutano wa mwaka uliofanyika Qadian, India mnamo mwaka 1925. Hotuba yenyewe ilipewa jina la *Minhaajut Taalibiin*, ikiwa na maana ya Njia ya Muongozo kwa tafsiri isiyo rasmi.

Endelea uk. 11

Siku ya Masihi Aliyeahidiwa as - 2017

Kutoka uk. 12

alikuwa akiwapatia nasaha ambazo kimsingi zinabeba dhima kubwa kwa wanajamaat walioungana nae na wale wanaoendelea kuingia na kujiunga katika silsila hii:

Katika kuadhimisha siku ya Masihi Aliyeahidiwa ambayo hufanyika ifikapo Machi 23 ya kila mwaka, Khuddamul Ahmadiyya wa mkoa wa Dar es salaam walitangulia kushiriki katika zoezi maalumu la matembezi ya baiskeli katika maeneo mbalimbali ya Manispaa za Ilala naTemeke.

Matembezi hayo ambayo yalihusisha zoezi la ugawaji wa vipeperushi vilivyobeba ujumbe wa Amani kutoka Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, yaliwashirikisha pia viongozi mbalimbali wa Tanzimu ya Khuddamul Ahmadiyya akiwamo Sadri sahib, Bw. Ramadhani Nauja.

Wakiwa wamevalia vizibao maalumu (reflectors) vya rangi ya kijani na machungwa vikiwa na michirizi mitatu ya kijivu inayong'aa upande wa kifuani hadi mgongoni, msafara wa Khuddam uliondoka katika viunga vya Masjid Salaam baada ya maombi yaliyoongozwa na Amir na Mbashiri wa Jamaat Ahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry, msafara wa Khuddam uliingia barabara ya Bibi Titi Mohammed mnamo saa 3:00 asubuhi kuelekea barabara ya Lumumba wakiongozwa na gari mbili, moja ilitangulia mbele na nyingine ilibaki nyuma kuhakikisha hali ya usalama kwa waendesha baiskeli wetu.



Sehemu ya Khuddam wakianza msafara wa zoezi la mbio za Baiskeli na ugawaji wa vipeperushi lililofanyika tahere 19/3/2017, siku chache kabla ya maadhimisho ya siku ya Masihi Aliyeahidiwa.

Kutoka Mtaa wa Lumumba, msafara ulipitia barabara ya Uhuru ambapo zoezi la ugawaji vipeperushi lilifanyika kwa takribani dakika 10 likiongozwa na Sadri Sahib. Baadae msafara ulisimama katika soko la Karume kisha Keko ambapo watu kadhaa walijitokeza kutaka kujua lengo la msafara wetu ambao kwa muda wote wa safari zilisikika sauti za Takbira na Tashahudi kutoka kwa vijana waliokuwa na hamasa ya aina yake.

Baadae msafara uliendelea safari hii ukipita katika barabara ya Changombe, Kilwa Road, Gerezani, Stesheni na baadae kurejea katika barabara ya Bibi Titi Mohammed yalipo Makao makuu ya Jamaat.

Moja ya matukio ya kukumbukwa ni kitendo cha askari wa Barabarani wakishirikiana na Polisi wa Usalama kuusimamisha msafara wa waendesha baiskeli wetu katika eneo la BP wakidhani kwamba pengine tulikuwa katika maandamano fulani. Baada ya mazungumzo ya muda mfupi na viongozi wa Khuddam msafara uliruhusiwa huku Polisi wakifuatilia nyuma hadi Masjid Salaam kuhakikisha kuwa hapakuwa na ajenda nyingine yeyote zaidi ya matembezi ya Amani.

Tukio hilo la uendeshaji baiskeli liliwachukua Khuddam kiasi cha saa moja na dakika 10 ambapo walikamilisha umbali wa Kilomita 10.73 za kuzunguka katika barabara za manispaa ya Temeke na Ilala ambazo zimekuwa na changamoto nyingi kwa waendesha baiskeli kutokana na uwepo wa magari mengi pamoja na uendeshaji usiozingatia kanuni za usalama wa barabarani unaofanywa na madereva wengi.

Kitaifa na kimkoa, maadhimisho ya Siku ya Masihi Aliyeahidiwa na Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waisalamu Waahmadiyya Ulimwenguni Hadrat Mirza Ghulam Ahmad a.s yalifanyika katika viwanja vya Jamaat katika eneo la Kitonga siku ya Jumapili.



Sehemu ya Khuddam walioshiriki mbio za Baiskeli na ugawaji wa vipeperushi wakiwa kwenye picha ya pamoja na Amir Jamaat Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry kabla ya kuanza kwa zoezi hilo

KUTOKA MEZA YA MHARIRI

Njaa yatishia uhai wa somalia

Taifa la Somalia ambalo limekuwa katika vita na misukosuko mingi ya kijamii kwa hivi sasa linakabiliwa na njaa. Sawa na taarifa ya shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) zaidi ya watu milioni 17 katika pembe ya Afrika wapo katika hatari ya kukabiliwa na njaa na hivyo wanahitaji msaada wa chakula haraka iwezekanavyo.

Toka kuanguka kwa utawala wa Mohammed Siaddi Barre, Somalia haijapata kupumua. Limekuwa ni taifa la mapigano miaka nenda miaka rudi na Serikali kwa hivi sasa inapambana na kikundi cha Al Shabab. Ukame ulioikumba Somalia hivi sasa unatisha kwani ni kwa miaka mitatu mfululizo wananchi wa Somalia hawajapata mvua.

Licha ya wananchi kutokuwa na chakula wanyama, ngamia na mbuzi waliokufa wametapakaa sehemu zote za nchi hiyo.

Tunao wajibu mkubwa wa kuwasaidia ndugu zetu hao kwani maumivu ya binadamu yeyote ni yetu pia. Aghalabu mashirika ya misaada ya kimataifa hutanabahi wakati hali imekwishakuwa mbaya sana. Tusianguke katika mtego huo wa kutafuta fimbo wakati tumekwishaumwa na nyoka.

Utandawazi

Ni kutojua tu. Lakini wazo la Utandawazi lililetwa na Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alipotuunganisha na kuondoa mipaka inayotokana na kabila, lugha, utamaduni na kutufanya kuwa kitu kimoja. Tunamshukuru Allah ya kwamba hali hii imerudishwa duniani na mwana wa kiroho wa Mtume (saw). Jumuiyya ya Ahmadiyya imeleta undugu na ukaribu wa aina yake. Kijana wa Kiahmadiyya kutoka nchini Nigeria Ilumoka Taofiq aliwasiliana na Naib Sadr Khuddam kanda ya ziwa Bw. Yusuf Mgeleka; katika mawasiliano hayo Bw. Ilumoka alimueleza Naib Sadr kanda ya ziwa kuwa angependa kutembelea Tanzania. Hii ilitokana na mawasiliano aliyokuwa nayo Bw. Ilumoka na rafiki yake aliye Amerika ambaye alimshauri ya kwamba nchi nzuri ya kuitembelea katika Afrika ni Tanzania.

Mipango ilifanyika na Khuddam huyo kutoka Nigeria aliyezaliwa mwaka 1995 akawasili Dar es salaam na kupokelewa na uongozi wa Khuddam. Akiwa hapa nchini alionana na Ameer na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry pia alitembelea sehemu za kuvutia kama vile Morogoro kwenye mbuga za wanyama n.k.

AkizungumzanaMapenziyaMunguBw.Ilumoka alisema ya kwamba alikuwa amefurahishwa sana na khulka na tabia za Watanzania ambao walionesha ukarimu na mapenzi makubwa. Akizungumzia juu ya Jamaat Ahmadiyya huko Nigeria alisema; "Kwa msaada wa Allah Jamaat nchini Nigeria ina shule za msingi 40 na shule za Sekondari 30". Tukizungumzia juu ya mambo ya uandishi na kuendeleza fasihi ya Kiafrika Ilumoka alisema Tanzania ina bahati ya kuwa na lugha moja ya taifa Kiswahili. Alisema ya kwamba katika Nigeria kila kabila lina lugha yake kwa mathalani Kihausa, Kiyoruba, Fulani, Igbo, n.k.

Tukizungumzia juu ya waandishi maarufu wa fasihi ya Kiingereza, aliweza kuwataja akinua Chinua Achebe na Wale Soyinka ambao wameiletea sifa kubwa Nigeria. Kijana huyo akisha toka Tanzania ataelekea Afrika ya Kusini na hatimaye Montrio Canada ambapo anakwenda kusomea shahada ya kwanza ya Uhandisi.

Muongozo kwa Wabashiri na viongozi wa kiofisi

Kutoka uk. 12

kwamba ni jukumu lao kuwaonyesha heshima na wahakikishe kwamba watu wengine wanawaheshimu Wabashiri. Wanatakiwa kufanya kazi kwa pamoja katika masuala ya Ucha Mungu na Utawa.

Inaonekana katika kila migogoro midogo midogo kati ya Raisi, Mbashiri na viongozi wengine, shetani anaingiza magomvi na anajaribu kuteteresha hali ya Ucha Mungu wa kila anayehusika. Wale watu ambao Maraisi na Wabashiri wanakutana nao kwa lengo la kubadili hali zao za imani, wanajaribu kuingiza tofauti kati ya Marais na Wabashiri na wanachochea ugomvi kati yao kwa kuwaambia kwamba tumepotoshwa na fulani. Mwisho hali hiyo inazalisha wasiwasi miongoni mwa watu. Masih Aliyeahidiwa (a.s) alisema hakuna Jumuiya itakayoendelea kubakia kama jumuiya ikiwa ndani yake kuna hali ya mashaka, unafiki na kutafuta makosa ya wengine.

Alisema tunatakiwa kuwa wamoja kama vile tunavyojua kwamba muungano wetu una lengo moja tu. Hivyo tunatakiwa kuongeza hali yetu ya uadilifu, ambayo inaweza ikafikiwa kwa kuwa na upendo, udugu na kuhurumiana.

Huzur alisema kwamba Wabashiri na viongozi wachukue tabia ya kufunika makosa ya wengine na kuonyesha huruma na msamaha na wawe mfano wa kuigwa katika kudhihirisha khulka hizi. Wasiwe wenye kupata hasira kwa mambo madogo kabisa na matokeo yake kujenga husda.

Huzur alifafanua kwamba kwa kutoa maelekezo haya, Mungu Apishie mbali, haina maana kwamba kuna migogoro iliyoenea sana kwa ujumla katika Jamaat kati ya Wabashiri, Maraisi na Maamiri. Hivyo sivyo kabisa. Kuna matukio machache tu ya aina hiyo ambayo yanaletwa kwa Huzur (atba) kila mwaka. Huzur (atba) alisema sababu inayomfanya ayaelezee mambo haya kwa uwazi ni kwamba Maraisi na Maamiri na Wabashiri wengine pia watambue upana mkubwa wa majukumu yao. Na ili kama kutatokea tofauti yoyote kati yao ziweze kutatuliwa haraka iwezekanavyo. Mwishoni waelewe kwamba wana lengo moja na wanahitaji kufanya kazi sambamba ili kutimiza majukumu yao ya kuwafundisha na kusaidia kuwarekebisha Wanajumuiya. Kama ambavyo Masihi Aliyeahidwa a.s wakati fulani aliwahi kusema, kazi ambayo inahitaji kufanywa kwa mikono miwili haiwezi kufanywa kwa kutumia mkono mmoja tu.

Mafanikio yetu yanategemea ushirikiano wetu na kufanya kazi kwa pamoja kufikia lengo moja. Mtu mmoja anaweza kufanya nini, aidha iwe katika mambo ya kidunia au ya kidini kulinganisha na Jumuiya kubwa inayofanya kazi mkono kwa mkono kufikia lengo moja? Kamwe Amiri asitekeleze amri zinazotokana na matakwa yake tu, wala Mbashiri asiyaone mawazo yake yote kuwa ni sahihi yasiyoweza kukataliwa. Jukumu la Mbashiri ni kusaidia kufundisha na kurekebisha Jamaat na hivyo kiwango cha Ucha Mungu cha Mbashiri kiwe ni cha juu zaidi kuliko cha wanajumuiya wengine. Kuweka kiwango hiki bila shaka kutaweka kiwango fulani cha heshima kwa Wabashiri kutoka kwa wanajumuiya kwa ujumla. Amiri akiwa ndiye kiongozi wa mambo ya kiutawala katika nchi yake ana jukumu la kuhakikisha mfumo na utawala unaendelea vizuri na ni mwakilishi wa Khalifa katika muktadha huu. Jukumu la Mbashiri ni kujitahidi kuboresha hali ya kidini na kiimani ya wanajumuiya na ni mwakilishi wa Khalifa katika muktadha huu. Hivyo, Maamiri, Maraisi na Wabashiri wanapaswa wote kushirikiana chini ya jukwaa la umoja ili kufanikisha lengo hili.

Huzur amesema tena atarudia kwamba: Ni jukumu la Maamiri wote, Maraisi na Viongozi kuheshimiana wao wenyewe na kupandikiza heshima katika jamaat kwa Wabashiri wote na waliojitolea wenyewe wakfu maisha yao. Hili pia litawahamasisha vijana kupenda kujitolea maisha yao kwa ajili ya kuitumikia imani. Bila shaka mtu huwa anajitolea maisha yake au anakuwa mbashiri kwa ajili ya kumridhisha Mungu. Lakini hata hivyo wakati fulani watoto na vijana huwa wanahitaji motisha unaoonekana kuwahamasisha mwanzoni kuchukua hatua taratibu za kujitolea maisha yao yote. Wanapoelewa kikamilifu lengo hasa la kujitoa kwao maisha, basi maendeleo ya kiroho yanapatikana na wanaachana na mambo ya kidunia.

Kwa hiyo Maamiri wote, Maraisi na Viongozi wakae na Wabashiri na waliojitolea wakfu maisha yao kwa huruma ya hali ya juu na ushirikiano ili mfanye kazi yetu ya kupata Wabashiri wapya kuwa rahisi zaidi. Tunahitaji Wabashiri wengi zaidi na wakujitolea wakfu maisha yao na hivyo ni lazima kabisa kwamba tujenge heshima na kuangalia katika mioyo ya wote.

Huzur (atba) alisema anapenda kuwaambia vijana wote waliojitolea wakfu maisha yao na Wabashiri wanaofanya kazi kwamba bila kujali kama dunia inawapa heshima au la, kama Amiri, Raisi, kiongozi au hata mwanajumuiya yeyote anawapa heshima itakiwayo au la, ni lazima katika hali yoyote watimize ahadi yao ya kujitoa wakfu waliyoifanya na Allah Mwenyezi. Wabashiri wamuelekee Mungu na kamwe wasiielekee dunia kwa matatizo yao yote. Kama kiongozi hawatendei sawasawa basi badala ya kulieleza hilo kwa watu wengine, Mbashiri awasilishe matatizo yake kwa Mungu katika maombi. Mbashiri asikhofu kuhusu watu bali ajiombee tu kwa Mungu pekee. Bila shaka, aliyejitolea wakfu maisha yake atafanya kazi ya Jamaat maisha yake yote wakati viongozi wanachaguliwa kwa vipindi vifupi. Kama kiongozi hafanyi kazi zake sawasawa na analeta tu matatizo, cha kufanya mbashiri ni kuomba kwamba kiongozi huyo awe katika njia sahihi au kwamba Mungu Mwenyezi amtenge kiongozi wa aina hiyo.

Hazur (atba) aliwaelekea Wabashiri na viongozi na kusema kwamba kama wanategemea wanajumuiya majumbani mwao waache kusengenya viongozi, basi Wabashiri na viongozi, wao kwanza wanapaswa kuhakikisha usengenyaji wa viongozi hautokei katika majumba yao wenyewe.

Viongozi wote na hasa Maamiri na Maraisi wa nchi, ni lazima daima kuwatendea wanajumuiya kwa upendo na mahaba. Ni lazima wakumbuke kwamba uongozi huu ni Baraka pekee za Allah Mwenyezi na hawana haki ya kuudai. Kwa hiyo, ni lazima watekeleze dhamana hii ambayo Khalifa wa zama amewapa kwa upole wa hali ya juu. Sawa na Hadithi moja, Mtume Mtukufu (s.a.w) daima alikuwa akiwasalimia watu kwa tabasamu hivyo mfano huu bora wa Mtume mtukufu (s.a.w) ni lazima daima uzingatiwe.

Baadhi ya watu wanalalamika kuwa mambo yao huwa yanapelekwa kwa viongozi wa Jamaat lakini miezi inapita na hawapokei majibu yoyote ya utekelezaji wake. Huzur (atba) amesema kwamba amelizungumzia hilo hapo kabla mara kadhaa pia kwamba mambo yasicheleweshwe kwa muda mrefu bila sababu na yatatuliwe haraka iwezekanavyo. Kama kesi fulani inahitaji muda zaidi basi wahusika wapewe taarifa ya maendeleo na maswali yao yapokelewe.

Mtume Mtukufu (s.a.w) ametukumbusha tusione kitendo chochote cha wema ni kidogo kwa sababu hata kumsalimia mtu kwa moyo mkunjufu ni tendo la wema. Kama viongozi watawasalimia wanajumuiya kwa tabasamu na moyo mkunjufu, hilo pekee litaondoa nusu ya huzuni zao.

Kila tendo na uamuzi wa kiongozi lazima lifanyike huku ikiingizwa khofu ya Allah, kushika upole na kutimiza matakwa ya haki. Mtume Mtukufu (s.a.w) safari moja alisema kwamba Allah Mwenyezi kamwe Hatamuacha mtu aingie peponi ambaye amepewa majukumu kwa ajili ya watu lakini anapuuza majukumu yake. Mtume Mtukufu (s.a.w) katika tukio jingine alisema kwamba katika Siku ya Hukumu, mtawala mwenye haki atakuwa ndiye mwenye kupendwa zaidi na aliye karibu zaidi na Mungu Mwenyezi na mtawala asiye na haki atakuwa mbaya kuliko wote mbele ya Allah Mwenyezi na atawekwa Naye mbali kabisa.

Hivyo, viongozi ni lazima watekeleze majukumu yao na hili linawahusu pia tanziim zote.

Sababu kwa nini Hazrat Musleh-e-Mau'ud (ra) alianzisha tanziim hizi ilikuwa ili kila mwanajumuiya aweze kufikiwa. Amir wa nchi, Maraisi wa matawi na Tanziim ni lazima wote wafanye kazi kwa kushirikiana na hili litaongeza maendeleo ya jumla ya Jamaat kwa wingi.

Viongozi ni lazima waonyeshe ujasiri wa hali ya juu kabisa na hata kama lawama iwekwe juu yao, wasitafute kulipiza kisasi hasa na badala yake wajichunguze wao wenyewe kama ni kweli au hapana kwamba kosa hilo wanalo na wajirekebishe. Hili pia linaingia katika mahitajio ya haki na usawa.

Kila mwanajumuiya pia ni lazima ajaribu kuongeza kiwango chake cha Taqwa kwani na wao pia wameagizwa kusaidiana katika Taqwa na uchaMungu. Kila mwanajumuiya ni lazima atimize jukumu lake kuhusiana na utii kwa sababu mfano wao wa utii sio tu kwamba utawawezesha kuimarisha muungano wao na Jamaat lakini pia utaviwezesha vizazi vyao kubaki vimeungana nayo. Kama viwango vya Taqwa na UchaMungu wa vizazi vijavyo vitakuwa ni vya juu basi bila shaka viongozi wa baadae watakuwa na viwango vya juu vya Taqwa na UchaMungu. Hivyo, wanajumuiya wayaingize maagizo ya Mtume Mtukufu (s.a.w) katika mioyo yao na pia katika watoto wao kwamba waonyeshe utii katika kila hali. Mtu aombe daima kwamba Allah Mwenyezi Awaweke viongozi wa aina ile ya kwamba watawatendea kwa upendo na huba na wawaombee na wao pia wawe na upendo kwao na pia wawaombee. Mtume Mtukufu (s.a.w) alisema katika tukio moja kwamba Allah Atagawa Rehema zake Siku ya Hukumu kwa wale wanaopendana kwa ajili Yake.

Huzur (atba) aliomba kwamba Allah Mwenyezi Amuwezeshe kila mmoja kutimiza majukumu yake aliyoagizwa alipoingia kwenye Jamaat ya Mfuasi Mkereketwa wa Mtume Mtukufu (s.a.w) na wadumu katika matarajio aliyo nayo kwao. Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) siku moja alisema kwamba Allah Mwenyezi Anataka kuanzisha Jumuiya ambayo itakuwa ni mfano wa Taqwa na Ucha Mungu. Viwango vyao vya ukweli na upole ni lazima viwe vya hali juu sana na ni lazima wawe wenye asili ya usafi na wajiepushe na mikutano ambapo watu wanakejeliana na kukashifiana.

Ninamuomba Allah Mwenyezi Amuwezeshe kila mwanajumuiya kufanya namna hii na awe mpokeaji wa Baraka za Allah Mwenyezi. Amin.

Dhambi zimetamalaki

Kutoka uk. 9

Je, kweli Dunia imejaa Dhambi au Shetani Ametamalaki? Akilijibu swali hili, Khadhrat Khalifatul Masihi wa Pili r.a, anasema:

Uhakika ni kwamba, kuna matendo mema mengi zaidi duniani kuliko maovu au dhambi. Mwanadamu huyumbishwa na mtazamo wenye kutatiza wa hali ya mambo na kusahahau kwamba Ulimwenguni mambo yaliyo mema ni mengi zaidi kuliko madhambi. Mtazame mwizi kwa mfano. Ni kweli anaiba na kutenda dhambi. Lakini kinyume na tendo la wizi, mtu huyu hufanya matendo mengi yenye wema ndani yake. Pengine hukutana na kusalimiana na watu kwa bashasha. Huwa na silika nzuri na huwasaidia wasiojiweza. Anawatunza vizuri wazazi wake na kuwajali. Ukitafakari kwa ujumla wake, utagundua mtu huyu anafanya matendo mema mengi kuliko dhambi ya kuiba aliyoifanya hapo kabla. Kwa mtazamo huu, utagundua wema ukiuzidi ubaya kwa kila jiha.

Pia, ukichunguza hali binafsi za watu, utagundua kuwa wanafanya matendo mazuri zaidi kuliko madhambi. Kiwango cha matendo mema au dhambi kwa yakini huupa wema nguvu zaidi kuliko dhambi. Tena zaidi ya hapo. Kwanini watu huwa na mtazamo wa jumla kuwa kiwango cha matendo maovu ni kikubwa? Mtazamo huu ni matokeo ya mambo mawili makubwa. Jambo la kwanza ni kwamba, iko bayana kabisa kuwa kiurasmi idadi ya waaminio na wale wasioamini, kwa hakika wasio waaminio utakuta ni wengi zaidi kwa idadi kuliko waaminio. Jambo la pili ni hili kwamba, watu wengi wana mapungufu haya na yale matendo yao. Kwa ajili hiyo, kiwango cha maovu au madhambi kinaonekna kikubwa. Lakini hiyo si sahihi. Mambo hayo mawili hayatoshi kuthibitisha kuwa maovu yametamalaki katika dunia.

Kwa hakika, wanaweza kuwepo watu wasio amini dini. Lakini idadi ya wasio amini dini wenye kuelewa ukweli na kuvutiwa na dini ni kubwa zaidi ya inavyoonekana kijuu juu. Wale wanaoitwa hawaamini dini mara nyingi wanakuwa hawajajitathimini hali zao za imani. Wengi wao huenda wakawa si makafiri machoni pa Mungu. Zaidi, Mungu atawapa nafasi ya kujichunguza na kuamua. Au kama hili halitokei, baadhi ya matendo yao ambayo waliyafanya kwa uhuru na kwa kukusudia yatapimwa kulingana na faida ya kimaadili. Sasa matendo yao yakipimwa kwa namna hiyo, tunawezaje kusema kuwa wengi wao wataonekana kuwa ni watu wema na wangapi wataonekana kuwa waovu?

Kwa ujumla tunaweza kusema kwamba imani imetamalaki zaidi katika dunia kuliko uovu.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

Mapenzi ya Mungu

Jam2/Raajab 1438 AH | MACHI 2017 | Amman 1396 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Jabir r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Kuna mambo matatu ambayo yakiwemo katika mtu, Allah Atamweka chini ya ulinzi Wake na kumwingiza Peponi. Nayo ni haya: Upole kwa wanyonge, huruma kwa wazazi na kuwafanyia hisani walio chini ya mamlaka yake. (*Tirmidh*)

Khalifa Mtukufu atoa muongozo kwa Wabashiri na viongozi wa kiofisi

Na Mwandishi Wetu,
Dar es Salaam

Katika Hotuba ya sala ya Ijumaa ya tarehe 10/03/2017 Hadhrat Khalifatul V (Kiongozi wa waaminio) (atba), aliwakumbusha Wabashiri na Viongozi wengine wa kiofisi juu ya haja ya kutekeleza majukumu yao kwa ushirikiano. Baada ya kusoma Tashahhud na Surat Fatihah, Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alisema:

Kwa fadhila za Allah Mwenye Enzi Jamia Ahmadiyya zinaanzishwa katika nchi mbalimbali ulimwenguni kote. Wabashiri wanahitimu kutoka huko na wamekuwa wakipangiwa kazi mbalimbali. Hapo awali Jamia Ahmadiyya ilikuwa inapatikana Qadian na Rabwah tu. Hivi karibuni yalifanyika mahafali ya pamoja ya wahitimu wa Jamia Ahmadiyya kutoka Uingereza na kutoka Canada. Wahitimu hawa wamechagua kujitolea maisha yao kwa ajili ya kuhudumia imani, ijapokuwa wamezaliwa katika mazingira ya nchi za Magharibi. Wengi wao kama sio wote wamo katika mpango wa Waqfu-Nau.

Mbali ya Rabwah na Qadian, Jamia Ahmadiyya pia zimeanzishwa katika nchi za Uingereza na Ujerumani, ambapo wanafunzi kutoka Ulaya wanapata nafasi ya kusoma huko. Kwa undani zaidi, Jamia Ahmadiyya Canada imepata hadhi ya kutambulika kama taasisi ya elimu kiserikali na imefanya wanafunzi kutoka katika nchi mbalimbali kupata nafasi ya kujiunga. Kuna Jamia Ahmadiyya katika nchi ya Ghana, ambapo mwaka huu Shahidi (wanafunzi wa mwaka wa mwisho) watahitimu. Pia kuna Jamia Ahmadiyya katika nchi ya Bangladesh na Jamia Ahmadiyya katika nchi ya Indonesia ambazo zimeongezwa ili kutoa mafunzo ya Ushahidi (hii ni Shahada ya miaka saba ili mtu awe Mbashiri).

Wakati wabashiri hawa vijana wanapoanza kazi zao huwa wana maswali ya aina fulani katika vichwa vyao na sababu ya kuhututubia hapa ni kwa sababu viongozi wa Jamaat wanatakiwa wafahamu kuwa ni muhimu kufanya kazi pamoja nao kwa maelewano, hivyo ndio maana Wabashiri na viongozi wanatakiwa kushirikiana kwa pamoja; hususan Maraisi na Maamiri (Maraisi wa Jamaat wa nchi).

Wakati fulani kutokubaliana kunaweza kukatokea na kwa kawaida ni kwa sababu ya kutoelewana na kunaweza kusababisha misuguano kati ya pande mbili. Inaweza ikatokea kwamba wakati fulani Mbashiri akafikiria mpango wa malezi na akataka kuutekeleza mpango huo ndani ya Jamaat yake, hata hivyo ikatokea Sadr Sahib (kiongozi wa Tanziim) asikubaliane nae. Au inaweza ikatokea kwamba kwa kukaa kwenye uongozi kwa muda mrefu, Sadr Sahib akafikiria kwamba mipango yake ni sahihi na Mbashiri anatakiwa kufanya kazi chini ya mipango hiyo.

Badala yake, katika mikutano ya wazi anaweza akataka majibu kutoka kwa Mbashiri kwa njia isiyofaa. Inawezekana Mbashiri asipendezwe na tabia hii na pia akalipiza. Ingawaje ninapenda kuwashauri Wabashiri kwamba wanatakiwa kuwatii wale wote waliokuwa na mamlaka juu yao na wanatakiwa kuonyesha utii wa hali ya juu kabisa kwa kubakia kimya. Vilevile ningependa kuwaasa Masadraan, Maamiri na Maraisi na kuwakumbusha

Endelea uk. 11

Siku ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.-2017

Mbio za Baiskeli za Khuddam zawa kivutio

Na Ayoub SADI- Dar Es Salaam.

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania, mwishoni mwa mwezi huu imefanya maadhimisho ya Siku ya Kumbukumbu ya Mwanzilishi wa Jumuiya, Hadrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, katika viwanja vya jamaat vilivyopo katika Viunga vya Kitonga, Dar Es Salaam.

Siku hiyo maalumu hujulikana kama Siku ya Masihi Aliyeahidiwa ambayo kikalenda, hufanyika kila ifikapo tarehe 23 ya Mwezi Machi, kila mwaka. Wanajamaat hukutana na kukumbushana malengo, shabaha na dhumuni la kuanzishwa kwa jamaat hiyo miaka takribani 127 katika kijiji kidogo cha Qadian, nchini India.

Katika maadhimisho ya mwaka huu ambayo yamebeba sura ya Kitaifa, wanajamaat kutoka katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Dar Es Salaam wakijumuisha Khuddam, Ansar, Lajna, Nasrat na Atfalul Ahmadiyya wapatao 450 walihudhuria na kushiriki na kupata fursa ya kukutana na kujadiliana mambo mbalimbali ya kidini na maisha kwa ujumla wake.



Amir na Mbashiri Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akitoa hotuba katika maadhimisho ya siku ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. yaliyofanyika Kitonga Dar es Salaam.

Kama ilivyo ada na desturi za Jamaat, hotuba mbalimbali zilitolewa na Viongozi wa jamaat bila kusahau mashairi yaliyosomwa kwa hisia kali ikiwa ni kusherehesha dhumuni la maadhimisho yenyewe na kuwakumbusha wanajamaat namna ambavyo wanatakiwa kuyaweka katika vitendo mafundisho na malengo ya kuanzishwa kwa jamaat ili tuweze kuhesabiwa miongoni mwa wateule wa Mwenyezi Mungu.

Baada ya hotuba, mashairi na mawaidha mbalimbali, wageni na wanajamaat walipata fursa ya kuuliza maswali mbalimbali ambapo majibu yalitolewa papo kwa hapo kutoka kwa wataalamu wa Jamaat na hivyo kufaidika.

Kihistoria, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s alianza kuchukua Baiat rasmi mnamo tarehe 23 Machi mwaka 1889 katika kijiji kidogo cha Ludhiana ambapo mtu wa kwanza kabisa kuweka mkono wake na kujiunga na Jamaat Ahmadiyya alikuwa ni mwanafunzi wake mtiifu na ambaye baadae alikuwa Khalifa wake wa Kwanza, Al-Haaj Maulvi Hakeem Nuruddin. Siku hiyo, jumla ya watu wapatao 48 walijiunga katika jamaat Ahmadiyya na kuandika historia ya kipekee na yenye kukumbukwa mno na wanajamaat Ahmadiyya ulimwenguni kote.

Kwa kawaida baada ya kukubali Baiat za watu waliojiunga naye kwa kukubali kwamba yeye ni Masihi wa zama hizi, Hadrat Mirza Ghulam Ahmad a.s

Endelea uk. 10